# MSOMO YA BIBLIA YA HABARI NJEMA

## Injili ya Luka kwa mikutano ya nyumbani

## YALIYOMO


1. Bikira achukua mimba Luka 1:26-38
2. Wachungaji katika machungani Luka 2:8-20
3. Anna na Simeoni Luka 2:25-38
4. Yesu akiwa kijana Luka 2:40-52
5. Ujumbe wa Yohana mbatizaji Luka 3:7-20
6. Siku ya kwanza ya huduma ya Yesu Luka 4:31-37
7. Kufua samaki wengi Luka 5:1-11
8. Ni nani aliye na furaha ywa kweli? Luka 6:20-26
9. Mpende adui yako! Luka 6:27-38
10. Msingi wa maisha yako Luka 6:46-49
11. Mjane wa Nain Luka 7:11-17
12. Mwanamke ambaye alisamahe mengi Luka 7:36-50
13. Mfano wa mpanzi Luka 8:4-15
14. NItakufuata Luka 9:57-62
15. Jina katika mbinguni Luka 10:17-20
16. Msamaria mwema Luka 10:25-37
17. Kitu kimoja tu kinahitjika Luka 10:38-42
18. Samaki na Nyoka Luka 11:5-13
19. Tajiri mpumbavu Luka 12:13-21
20. Mmoja mwaminifu wengine sio Luka 12:35-48
21. Mkuyu tasa Luka 13:6-9
22. Mwanamke mlemavu Luka 13:10-17

23. Mlango mwembamba — Luka 13:22-30

24. Karamu kuu — Luka 14:12-24

25. Kondoo aliyepotea — Luka 15:1-7

26. Kijana mpotevu — Luka 15:11-24

27. Kijana mwigine mpotevu — Luka 15:25-32

28. Tajiri na Lazaro — Luka 16:19-31

29. Walikonywa kumi mmoja kaokoka — Luka 17:11-19

30. Mjane mwenye kushikiria — Luka 18:1-8

31. Ni nani mtakatifu? — Luka 18:9-14

32. Mtosho ushuru juu ya Mkuyu — Luka 19:1-10

33. Mfano wa mwisho — Luka 20:9-19

34. Sadaka ya mjane — Luka 21:1-4

35. Petero amdharau mkuue wake — Luka 22:54-62

36. Mirango ya Paradiso imefunguliwa — Luka 23:32-43

37. Matembezi kwenda Emau — Luka 24:13-35

38. Kwa Matafia yote — Luka 24:44-53

# 1. BIKIRA AZAA      Luka 1:26-38

Angalizo: Haya yote yalipotendeka, Mariamu alikuwa msichana kijana, labda chini ya umri wa miaka 20. Aliposua kuolewa na Yusufu seremara. Mapenzi nje ya ndoa yalikatazwa na Agano la Kale.

1. Je Mariamu alikuwa na tabia gani? – Je unatoa hitimisho gani kutoka somo mistari hii?

* Je Mairamu alikuwa na uhusiano wa aina gani na Mungu?

* Fikiria maisha Mariamu ya siku kwa siku katika kijiji kidogo cha Nazareti – Je kulikuwa na furaha na huzuni wa aina gani?

2. Kwa nini Mungu alimchagua huyu msichana mdogo kuwa mama wa mwanaye?

* Fikiria sababu mbalimbali ambazo zilimfanya Mariamu alifanya kama alivyofanya ktokana na salamu za malaikal (29)?

3. Je ni kwa sababau gani Mungu alimtuma Gabrieli kwa Mariamu?

* Soma mistari ya  32-33. Mariamu alijinfunza nini juu ya mtoto ambaye mwishowe atamzaa? Sema kwa maneno yako.

4. Mariamu alikuwa bikira. Je angeaminije tayari katika kuzaliwa na bikira wkati hakuwa na hakikishololote? (Kwa maneno mengine, kabla ya ishara yeyote ya mimba kuonekana katika mwili wake.)

* Kwa nini watu wengi siku hizi hupata shida kabisa kuamini kuzaliwa na bikira?

5. Katika injili ya Matayo tunaona kwamba Yusufu alikuwa na dhisa pia katika kuamini kuzaliwa na bikira. Kama Mairamu angalijua uchungu iliokuwa unmsubiri kama mama wa Yesu je unafikiri angalikubali wito huu?

6. Gabriel alisema mara mbili kuwa Mariamu alikuwa amepta neeema kutoka kwa Mungu (28,30). Neno  "neema" inamaanisha msamaha wa dhambi. Kwa nini Mariamu alihitaji wa dhambi?

7. Labda umejisikia kuwa matatizo yako ni magumu sana hata kwa Mungu kutatua. Soma mstari wa 37 na uitumie katika matatizo yako. Mstari huu una maana gani katika hali yako ya sasa?

8. Katika miaka thelathini na baadaye, Mariamu alisimama kando ya msalaba wa mwanae. Je alifikiri nini juu ya ahadi ya Mungu iliyoko katika msitari ya  32-33?

9. Kama Mungu angepkupa maisha yaliyojaaa neema, na wakati huohuo maisha yaliyojaa mateso kama ya Mariamu ungemjibu nini?

## 2. WACHUNGAJI MAKONDENI    Luka 2:8-20

TAZAMA: Wakati wa Yesu wachungaji walidharauliwa kwa sababu hawakuweza kutunza sabato. Kwa mfano hawakukubalika kuwa mashahidi katika mahakama. Katika Agano la Kale, malaika waliwatokea watu maalumu kama vile Abrahamu, Ezekieli na Danieli.

1. Fikiria juu maisha ya kila siku ya wachungaji katika milima ya Uyahudi. Walikuwa na furaha zipi na huzuni upi?

* Je unafikiria nini juu ya uhusiano katik ya wachungaji na Mungu, ambaye amri zake hakuweza kutunza?

2. Yerusalemu ulikuwa karibu na Bethrehemu, ukiwa na watu wengi waliokaa kule. Kwa nini malaika hawakuwatokea wale watu badala ya wachungaji?

3. Inasema katika mstari wa 9 malaika walipatwa na hofu kuu. Waliogopa nini?

* Unaogopa nini siku hizi? (Jibu katika moyo wako.)

4. Nini kiliwafanya wachungaji kuwa na furaha waliposikia maneno ya malaika (10-12)?

* Ebu sikiria malaika kusema mstari.10-11 kwako wewe. Je unafikiri ungeweza kuwa na furaha? kwa nini, kwa nini sio?

5. Wachungaji walifikiria nini waliposikia kuwa mwokozi aliyetarajiwa siku nyingi alikuwa amelala katika hori la ngome? (Hori ni sehemu ambayo ngombe wanakulia nyasi kavu.)

* Ingesikiaje kama ungeambiwa: "Mwokozi wa ulimwengu amelala katika sufuria ya kuogea?

6. Malaika walikuwa na sababu gani kufurahia juu ya kuzaliwa kwa mwanae katikati ya uchafu, baridi maadui na chembechembe cha magonjwa (13-14)?

* Kwa mwokozi kazaliwa katika hali hii?

7. Kwa nini Mungu alimwonyesha mtu mwingine mara tu arlipozaliwa?

8. Malaika waliwezaje kupata hori la ngombe katika ya usiku?

* Kwa misingi ipi wachungaji waliweza kutambua kuwa motto aliyelala katika hori la ngombe ni Kristo Bwana?

9. Ni nini kilichokuemo katika maneno ya wachungaji kilichompa faraja  Mariamu na Yusufu ambao walikuwa na usiku mgumu?

* Kwa nini Mungu alituma malaika kwa Mariamu na Yusufu – Kwa nini hatuma wachungaji badala yake?

10. Wachungaji waliwambia watu juu ya waliyoyaona na kusikia usiku ule wa Kristmas. Kwa nini wengine wote hawakwenda kumsujudu mtoto Yesu?

11. Ilichukua miaka 30 kabla ya Yesu kuwa maalufubecame – Wachungaji wangi wale walikuwa wamekuwa wakati huo. Maisha ya wachungaji yalibadilikaje baada ya kumwona Mwokozi? Ni nini hakikubadilika?

* Wachungaji waligundua nini juu ya uhusiano wao na Mungu kupitia kwa matukio haya?

HABARI NJEMA: Malaika waliimba juu ya amani na furaha usiku ule wa Kristmas. Amani na furaha, hata hivyo, gharama ambayo aliweza kulipa. Alianza kulipa katika hori la ngombe na akamaliza kulipa msalabani.

## 3. ANNA NA SIMEONI    Luka 2:25-38

KUMBUKA: Lija ya kwamba Mariamu na Yusufu walitoa makinda ya njiwa Hekaluni inaonyesha kwamba walikuwa masikini. Linganisha na Walawi.12:7-8. Watu wengi walisubiri Masiah wakati ule, lakini wangi wao walifikiri wangalionysha nguvu na mamlaka yake kwa mtu yeyote.

1. Fikiria aliyoyapitia Anna wakati mme wake alikufa baadya ya ndoa yao ya miaka sana. (36).

* Kwa nini Anna alitaka kuolewa, kama livyokuwa desturi siku zile- Fikiria sababu mbalimbali.

* Je maana ya maisha ya Anna ilikuwa kwa kipindi cha miaka yake ya 50-60 kama mjane (36-37)?

2. Unafikiri Anna alikuwa anaomba kwa ajili ya nini Hekaluni usiku na mchana mwaka hadi mwaka?

* Je mstari wae 38 unaonyesha nini juu ya imani ya Anna? (Alitaka ukombozi kwa minajiri gani?)

3. Ebu fikiria maisha aliyoishi Simioni hadi siku alipokutana na Yesu. Je furaha na huzini zake ilikuwa zipi (25-26)?

* Je ahadi ya Mungu kwa Simioni ilimaanisha nini (26)?

4. Inamaanisha nini kwa mzee kuwa na kitu cha tumainia siku za usoni?

* Je "kusubiri" kuna maana gani na  "imani"?

* Je kuna tofauti gani katika Masihi ambaye Simoni alimsubiri and Masihi ambaye watu wengi wanamsubiri? (tazama maelezo na mstari 25.)

5. Simioni angewezaje kumwona Kristo wa Bwana katika mtoto wa familia masikini?

* Why didn't all the other visitors to the temple see what Anna and Simeon saw?

6. Tazama somo hili kwa makini na jaribu kupata alama kuwa ni wokovu aina gani hawa wazee wawili waliomtazamia Masihi kuleta (25,31,32,38)?

* Unataka nini na zaidi sana kutoka kwa Yesu?

7. Ina umuhimu gani kwa mtu kusema kuwa yuko tayari kufa (29)?

* Ukitumia maneno ya Simioni katika maisha yako. Unaweza kusema jinsi alivyosema katika mistari 29-30?

8. Je kuna ujumbe gani mpya katika maneno ya Simioni yanafunua kwa Mariamu kuhusu motto wake (30-35)?

* Je upanga uliingiaje moyo wa Mariamu? (jibu linatoka nje ya somo mstari huu.)

9. Anna na Simioni hawakukutana na Yesu tena. NI kwa njia gani kuonana na motto Yesu kulibadilisha maisha yao? Nini kilibaki kama kilivyokuwa?

10. Je hawa watu wawili walikuwa na wito gani hadi kifo vifo vyao?

(* Katika siku zetu, watu wengi wana hamu katika karama ya unabii. Kwa nini Anna anitwa nabii wa kike? Tazana Mst.36.)

HABARI NJEMA: Kama umemwona Yesu kupitia neon la Mungu unaweza kusema kama Simioni: "Sasa Bwana umetimiza ahadi yako  na unaweza kumruhusu mtumishi wako aende kwa amani. Kwa macho yangu nimeuona wokovu wako."

# 4. YESU AKIWA KIJANA Luka 2:40-52

KUMBUKA: Watoto wa kiume wa Kiyahudi huwa wanaume wakiwa na umri wa 13. Mwisho Yesu alikuwa na ndugu zake wa kiume wanne na dada zake (Mathayo 13:55-56). Baba yake alikuwa seremara na alijifunza biashara ya baba yake. Hekalu ni mahali pekee ambapo Wayahudi waliruhusiwa kutoa kafara kwa ajili ya dhambi zao. Mungu aliahidi kuwa uwepo wake utakuepo pale.

1. Mariamu alitunza familia ambayo iliendelea kukua. Je unafikiria safari ya pasaka ya kila mwaka ilimaanisha nini kwake?

* Je ni maandalizi ya aina gani ambayo alikuwa nayo ili kuzesha kufanya safari ya majuma mawili?

2. Fikiria maisha ya kila siku ya mvulana Yesu kama mtoto wa kwanza katika familia ambayo iliendelea kukua.

* Ilikuwa na maana gani kwa mvulana Yesu kwamba aliweza kusafiri, pengine kwa mara ya kwanza kwenda Yerusalemu na wazazi wake?

3. Kwa nini Yesu hakuwaambia mapema wazazi wake kwamba asingali rudi nyumbani pamoja nao ?

* Zaidi ya sehemu zote, kwa nini Yesu alitaka kwenda Hekaluni?

4. Je mistari ya 46-47 inatuonyesha nini juu ya Yesu?

* Ni nini ambacho kilivutia huyu mvulana wa miaka ?

5. Kwa nini Yesu alishngaa kwamba wazazi wake hakujua alikwa wapi?

6. Kwa nini ilikuwa muhimu kwake Yesu kukutana na baba yake wa mbinugni Hekaluni badala ya mahali aikokuwa?

7. Je mstari wa 48 unatuonyesha nini juu ya Mariamu?

* Je Mariamu alifanyaje alipokosa kumwona mwanae miongoni mwao?

8. Je wazazi wa Yesu wajisikiaje waliposikia mvulana wao akijibu katika mstari wa 49?

* Je Yesu alitaka kuwafundisha nini wazazi wake kutokana na tukio hili?

9. Kulingana somo hili, lini tuna haki kuenda kinyumbe na wazazi wetu?

* Kulingana na somo hili, ni nini mapenzi ya Mungu dhidi ya kijana?

* Kulingana na somo hili, tunahitaji wa kuwatenda vijana wetu?

10. Je uhusiano wa Yesu na wazazi wake ulikuaje na watu wengine katika kipindi cha miaka 18 katikati ya tukio hili na kwanzo wa huduma yake ya hadharni (51-52)?

HABARI NJEMA: Sababu ambayo Yesu alipenda Hekalu imeandikwa katika Yohana 2:19-21. Kiongozi anaweza kusoma mistari hii.

# 5. UJUMBE WA YOHANA MPATIZAJI Luka 3:7-20

KUMBUKA: Yohana alikuwa na wazazi wake ambao walikuwa wazee ambao sasa walikuwa wamekufa tayari. Hakuwa na watoto na wala hakuoa. Yohana aliishi mahali pa upweke ambao ni jangwani.

1. Je Yohana alipata kuwa mtu wa aina gani kama kila mara alikuwa amezungukwa na marafiki?

* Fikiria wakati ambao umejiskia mpweke. NI mambo gani ya faida ambayo upweke ulileta katika maisha yako?

2. Yohana aliwaita wasikilizaji wake "wazao wa nyoka" (7). Kwa nini hata hivyo alikuwa maarufu kuliko Yesu?

3. Tazama maneno ya Yohana katika mistari ya 7-14. Tunawezaje kututmia mistari hii katika jamii yetu?

* Katika ujumbe wake ni nini kinachoma dhamiri yako?

* Dunia ingekuwaje kama kila mmoja angeishi kama vile Yohana anavyotwambia tuishi?

4. Linganisha ujumbe wa Yohana na ujumbe unaousikia katika mikutano na Kikristo. Kuna tofauti gani?

* Kama mtu angehubiri katika Usharika wako au katika kikundi cha Kikristo kama vile Yohana alivyohubiri, je unafikiri watafanyaje?

5. Mistari ya 4-6 inatwambia kuwa kazi ya Yohana ilikuwa ni kuandaa njia ya kuja Masihi katika mioyo ya watu. Ni kwa njia gani ujumbe mkali kama wa Yohana unaandaa njia kwa kuja kwake Yesu katika mioyo yetu?

* Kungefanyika nini kama Yohana nagalihubiri hivi: "Mungu anajua udhaifu wako na anakukubali jinsi ulivyo!"

6. Je Yohana alikuwa na uhusiano gani na Masihi aliyetarajiwa kuja? (15-17)?

* Kwa nini Yohana hatukutmia umaarufu wake kwa faida yake binafsi?

7. Yohana alimkemea Mfalme Herode kwa ajili ya dhambi aliyoifanya katika maisha yake ya siri (19-20). Kwa nini alitaka kuingilia uhusiano wa kimapenzi wa mfalme?

* Ni katika hali gani tunaweza kukema watu wengine kwa ajili ya dhambi yao ya usherati?

8. Yohana alikuwa tu umri wa  30 alipouawa gerezani. Maisha yake mafunpi yarikuwa ya maana gani?

* Ni kipindi gani ambacho kilikuwa cha furaha katika maisha ya nabii huyu?

9.Yesu alikuwa mmoja wapo wa wale ambao walisikia ujumbe wa Yohana mpatizaji. Alikuwa mti ambao ulizaa matunda mema. Kwa nini basi yeye "alikatwa na kutopwa motoni" (9)?

HABARI NJEMA: Ujumbe wa Yohana alikuwa wa Amri and onyo ambao ulileta ufahamu wa dhambi kwa wasikilizaji. Hata hivyo katika injli nyingine Yohana anatangaza jinsi Msihi atafanya na dhambi: "Tazama mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu” (John 1:29).

# 6. SIKU YA KWANZA YA HUDUMA YA YESU   Luka 4:31-37

KUMBUKA: Mwanaume aliyekuwa na roho pepo ndani yake ilikuwa kile tunaita "kupagawa". Kupagawa ni tofauti na kuwa na ugonjwa wa akili. Hii ina maana kwamba room mchafu anakaa katika myo wako kama vile Roho Mtakatifu anakaa katika moyo wa muumini. Roho mtakatifu hasa anamwingia mtu kupitia kwa kuabudu miungu,uchawi, waonaji, uponyaji wa dini za uongo, musiki aina fulani ya Musiki wa kishetani ambao ni wa viombo vya nguvu na makelele n.k. Mtu ambaye amepagawa anenda mara kwa mara katika " kifafa", analia kwa sauti isiyo ya kibinadamu na kila mara ana nguvu isiyo ya kawaida.

1. Je unaamini uwepo wa Shetani na mapepo?

* Kama umewahi kusikia masimulizi mbalimbali juu ya kupagawa na mapepo na megine, tafhadhali tushirikishe kwa kifupi sasa hivi.

* Kwa nini watu wengi wanaogopa giza, mapepo, roho wachafu na miungu?

2. Fikiria maisha ya kila siku ya huyu mtu aliye pagawa – fikiria hasa juu maisha ya familia yake na mahusiano mengine.

* Hii ilikuwa ni Sabato ya kwanza ambayo Yesu alishereheka kule Kapernaumu ambayo inamaanisha kwamba watu hawakuja sinagogi kukutana naye. Unfikiri kwa nini huyu mtu aliyepagawa na peopo mchagu alikuja huko hata kama alijua kuwa angepata "kifafa" wakati wowote?

3. Kwa nini mapepo hulia mara kwa mara wanapofika karibu na Yesu?

* Sema katika maneno yako yale ambayo roho mchafu alijua juu ya Yesu (34).

* Je romor mchafu alikuwa sawa juu yay ale yote alisema juu ya Yesu au la?

4. Kwa nini Yesu alizunmza na roho mchagu na wala si Yule mwanaume?

* Kwa nini Yesu akujibu swali ambalo roho mchafu alimuuliza (34-35)?

5. Kwa nini Yesu alimzadia Yule mwanaume alipagawa japo hakumwomba afanye hivyo?

* Pengine umesikia masimulizi juu ya mtu ambaye anatoa mapepo kutoka kwa mtu. Je kuna tufauti gani jinsi Yesu alitoa roho mchafu?

6. Ni kitu gani katika Yesu ambacho watu walishngaa? (32, 36)?

* Je maneno ya Yesu yana tofauti nay ale ya watu wengine?

* Ni kwa shida gani au kwa ajili ya mtu gani unahitaji maneno ya nguvu ya Yesu? (jibu moyoni mwako.)

7. Kulingana na somo hili, unaweza kusmea nini kwa mtu ambaye anaogopa giza, roho, mapepo ,sanamu, au nguvu za Shetani?

* Je unafikiri ni kwa kiwango gani Kanisa inawazaidia wale ambao wamefungwa na roho za ulimwengu?

8. Kwa nini Yesu alizanza huduma yake kwa tendo la namna hii?

9. Je kuna tofauti gani kati ya mtu ambaye ameanguka katika dhambi na mtu ambaye amebegagwa na roho mchafu?

10. (Majibu ya maswali ya mwisho yanatoka nje ya somo hili.)

* Je Yesu alipataje mamalaka ya kuamuru roho wachafu?

* Je htimaye Yesu anawezaje kuaribu Shetani na roho zake wachafu (34)?

* Hata ingawa alikuwa na mamlaka ya kuharibu roho wachafu, kwa nini Yesu aliharibiwa nao msalabani?

# 7. KUFUA SAMAKI WENGI      Luka 5:1-11

KUMBUKA: Petro alikuwa na mama mkwe (4:38-39), hii ina maana kwamba alikuwa na mke na watoto. Petero alikuwa mvuvi – kama hakupata samaki asingalikuwa na njia ya kuishi. Katika ziwa la Gennesareti walifua usiku (si mchana) na katika yale yasiyo na kiina kuliko maji marefu.

1. Kama miongi mwenu kuna aliye fanya kazi usiku, tafadhali tuambie unsikiaje asubuhi iliyofwata?

* Fikiria Petero alikuwa nafikiri nini alipoendelea kusafisha nyavu zake baada ya usiku wa kazi isiokuwa na mafanikioful (2)?

2. Kwa nini Yesu alipenda kuwa katika mashua alipowafundisha watu (3)?

* Unafiki ni kwa sababu gani Yesu alichangua mashua ya Petero kama chukua lake?

3. Petero alikuwa amesafisha nyavu zake. Na zaidi sana alikuwa hodari katika kufua samaki, ila Yesu hakuwa. Ni nini kilimfanya kufuata maagizo ya Yesu lija ya kuwa angejiabisha mbele ya wavuvi wengine (4-5)?

* Unafikiri nini: Je Petro aliamini kuwa angalipata samaki au hapana?

4. Kam Yesu angalikwambia ufanye jambo fulani ambalo unafikiri haliwezekani, ungemjibu nini?

5. Miaka michache iliyopita mashua ya kufua samaki ilipatikana katika ziwa la Gennesareti. Ilikuwa na urefu mita nane na upana wa zaidi ya mita mbili. Je ni smaki wangapi wenye uzito wa kilo moja ambao mashua mbili za namna hii wangebeba (7b)?

* Kulifanyika nini kwa samaka hawa wote?

6. Ni nini kinachokushangaza juu ya tamko la Petero katika muujiza huu?

* Ni dhambi gani ambayo Petro alikuwa nayo katika mawazo yake aliposema maneno yaliyo katika mstari wa 8?

7. Je Petro alijifuza nini juu ya utu wa Yesus kupitia kwa muujiza huu? (Tazama pia alivyo sunguza na Yesu katika mstari wa 5 na 8.)

* Ni nini kilicho mfanya Petero kuogopa?

8. Kwa nini Yesu alizungumza kama alivyozungumza katika mstari wa . 10 baada ya ukiri wa Petero?

* Je wavuvi wana kitu gani sawa sawa na mtu ambaye anahubiri injili?

9. Je Petro alikuwa na uhakika gaki kuwa familia yake wasingalihisi njaa baada ya kuwaacha ili kumfuata Yesu?

* Je una uhakika kuwa familia yako hawatatezeka ikiwa utaamua kumfua Yesu popote atakapo kwambia uende?

HABARI NJEMA: Simioni hakukosea alipofikiria kuwa mwenye dhambi hasinge kusogea karibu na Mungu mtakatifu. Alifahamu yale ambayo Agano la Kale lilisema: Mwenye dhambi ambaye anayesogea karibu na Mungu atakufa. Hii ndio sababu Yesu alihitaji hali ya Simioni ambayo alimfanya agope- aliachwa na Mungu alipokaribia kifo.

# 8. NI NANI ALIYE NA FURAHA YA KWELI?    Luka 6:20-26

KUMBUKA: Neno "mbarikiwa" maana yake ni kuwa "Furaha iliyo na kifani" katika lugha ya Kiyunani. “Matajiri” katika somo hili ni wale ambao wana kila kitu ambacho wanahitaji maishani: pesa, upendo, na afya. "Masikini" inamaanisha wale watu ambao hawakuwahi kuwa na hivi vitu wala kupoteza njiani. (Tafhadhali usichukulie neno "masikini" kumaanisha "masikini wa roho", Yesu hamaanishi hayo hapa.)

1. Je furaha ya kweli katika mtu  kulingana na somo hili?

* Je ni nini hasa kutokuwa na furaha katika somo hili?

2. Ni nini kulingana na Yesu ni hakika sehemu katika kuwa masikini? (Kwa sababu maana ya neno "masikini", tazama maelezo hapo juu.)

* Je nini pungufu kuwa tajiri? (Tazama maelezo hapo juu.)

* Katika vikundi hivi viwili ni kikundi gani unahesabika? (Jibu katika moyo wako.)

3. Watu wengi sana wana njaa duniani hawana chakula. Yesu anawezaje kuwaita wana furaha?

* Watu wengi katika jamii yetu wanatafuta upendo na kushukuriwa. Yesu anawezaje kuwaita wana furaha?

4. Fikiria hali Fulani mbayo ilikufanya ulie. Ungesikiaje kama Yesu angalifika kukutembelea na kusema: "Unafuraha wewe mbayo unalia sasa"?

* Fikiria mtu ambaye hajawahi kulia. Kwa nini ni vigumu kumwita mwenye furaha?

5. Ni kwa misingi gani Yesu alitamka kuwa wanafunzi wake ambao walikuwa wanalia walikuwa na furaha?

* Je wanfunzai wake walikuwa na furaha wakatika wanalia au baadaye wanakati watakapo cheka?

6. Kuna ubaya gani na utajiri, kulithika, furaha na kusemwa vema?

* Utafika lini mda wa matajiri, walivyo navyo na wanye furaha kulia?

7. Kwa nini wanaosema ukweli wanachukiwa, na kwa nini wanazungmziwa vema, wale ambao ni manabii wa uongo? (22,26)?

* Je unafikiri kuna watu hasa ambao wanafurahi na kusherehekea wanapotezwa na kulaumiwa (23)? Kama wapo, kwa nini nafanya namna hiyo?

8. Wana nini wale ambao ni masikini, wasivoy navyo, kulia na watu wenye kulaumiwa wanacho kwamba matajiri n.k hawana?

9. Kwa nini Yesu anawaita wanafunzi wake kuwa wana furaha na wala si watu wote ambao wanatezeka duniani (20)?

10. Na tuitumie mistari hii katika maisha ya Yesu. Jadili yafwatayo: Je Yesu alifurahi aliponinginia masalabani. Kwa nini? Kwa nini sio?

* Kwa nini Mungu akumpa Yesu faraja alipotezeka?

# 9. MPENDE ADUI YAKO! Luka 6:27-38

KUMBUKA: Ulipokuwa unasoma somo hili, fikiria juu ya juma lililopita – Ni kwa kiwango gani ulitimiza amri hizi katika maisha yako ya kila siku.

**Mistari ya 27-30**

1. Wengi wetu tunaweza kukubaliana kwamba kila mmoja wetu tunahitaji kuishi kama vile Yesus anafundisha hapa. Kwa nini ni vigumu kuishi hivyo?

* Je ingekuwa raisi kufuata mafundisho ya Yesu kama angesema: "Uwe mwema kwa adui zako"

2. Fikiria kuwa ungeweza kuanza kufwata sheria hizi ndani ya nyumba yako, shuleni ua kazini. Je unafikiri kutakuwa na mabadiliko gani, nyumbani kwako/Shuleni/kazini?

* Je unafikiri uhusiano wako na mtu ambaye humpendi ungeweza kubadilika kama ungemwombea (28b)?

3. Yesu alifwata amri zote hadi mwisho. Kwa nini bado alikuwa na maadui?

4. Je chuki huleta madhara gani kwa mwenye chuki?

**Mstari wa 31-38**

5. Kuna tofauti gani kati ya “Wana wa aliye juu” na “wenye dhambi” kama vile wanavyoelezewa katika mistari hii?

* Ni kwa njia gani unafanana na wana wa aliye juu nan i kwa njia gani unafanana na wenye dhambi?

6. Je wale wanaolalamika juu ya watu wengine kuwa hawawatambui wanaelewakaje vibaya (36-38)?

* Ni watu gani ambao wanahitaji upendo usio na mipaka zaidi ya wote ?

7. Mstari wa 35 unaelezea juu ya upendo wa Yesu kwetu hata kama tungekuwa maadui wake. Soma mtari huo na ujibu swali: Je nivigumu au raisi kwa mwanadamu kuamini katika upendo huo usio na vipimo?

8. Thawabu kubwa imea ahidiwa kwa wale ambao wanafwata amri hizi (35). Yesu alifanya na badala ya kupewa thawabu alisulubiwa. Kwa nini?

9. Je tunawezaje kujifunza kuwapenda maadui zetu?

* Wale ambao wameshindwa kuwapenda adui zao watawezaje kuwa wana wa aliye juu?

HABARI NJEMA: Kwa maana halisi ya neno, Ni Yesu tu ambaye ni mwana wa Mungu aliye juu. Aliwapenda maadui zake na kuwapenda hadi mwisho. Hakuchukua thawabu kweke yeye binafsi, ila anawapa wale ambao wanamwomba msamaha wa dhambi kwa ajili ya kutoweza kutunza amri hizi zote.

10. MSINGI WA MAISHA YAKO    LukA 6:45-49

1. Je Yesu anamsema nani katika mst.45?

2. Kuna mambo gani yana tabia sawa kati ya nyumba na maisha ya mtu? tafutata kwa wingi uwezavyo.

* Kwa nini watu wengi wanafikiria tu juu ya sehemu ya mbele ya nyumba/ maisha kuwa muhimu kuliko msingi?

3. Je kuna vitu gani ambao watu wanatengeneza ili kuweza kuweka msingi wa maisha yao?

* Kwa nini watu wengi hujenga maisha yao bila “kuchimba kwa kina” kwanza?

4. Yesu anamaanisha nini kwa kusema "mafuriko" au "mbubujiko" ambayo unaweza kukumba maisha ya mwanadamu?

* Je unawezaje kutawala hali kama maisha yako yatapiwa na “mafuriko” ambayo inakuogopesha?

5. Kulingana fumbo hili, "mafuriko" ambayo imepigwa katika maisha ya Wakritsto na wale wasio Wakristo. Kwa Wakaristo hawaachwi?

6. Fikiria kipindi ambacho maisha yako ulikumbwa na. Ushikiria nini wakati ule?

* Je maneno ya Yesu yalikuzaidiaje wakatika wa dhiki? tafathdhali tushirikishe.

7. Ni nini kitatendeka kwa mtu ambaye nyumba yake ikivunjika? (Atakuwa na maisha gani baada ya dhiki?)

8. Kutakuwa na sababu gani kwa mtu ambaye anasikia maneno ya Yesu lakini hatendi hivyo?

* Kuna nini ambacho kitamfanya mtu kuweka maneno ya Yesu katika vitendo?

* Je unaegemea upande gani katika vikundi hivi viwili? (Jibu katika moyo wako.)

9. Kuweka maneno ya Yesu katika vitendo ina´maana miongoni mwa mambo ambayo tuliambiwa kipindi kilochopita: Mpende jiarani yako. Je unaweza kuseoma kuwa maneno haya yamekuwa msingi wa maisha yako?

10. Neno "mwamba" lina maana nyingine zaidi katika Biblia. Paulo anasema katika 1.Wakorintho.10:4: "Mwamba ulikuwa Kristo." Je kuna tofauti gani kama ukijenga maisha yako katika amri za Yesu (Amri) au kama utajenga maisha yako katika Yesu mwenyewe (Injili)?

11. Yesu mwenyewe alishika mari zote. Kwa nini basi "mafuriko" yaliharibu maisha yako?

# 11. MJANE WA NAINI   Luka 7:11-17

KUMBUKA: Watu wanamwita Yesu Nabii Mkuu kwa sababu wanakumbuka jinni Elijah na Elisha wa Agano la Kale alimfufua mwana wa mjane kutoka wafu (16).

1. Fikiria sababu mbalimbali kwa nini watu wengi walitaka kuhudhuria mazishi haya (12).

2. Fikiria juu ya maisha ya huru mjane. Alikuwa na motto mmoja wakati kila mtu alitaka watoto wangi iwezekanavyo. Unafikiri ya familia hii ndogo yalikuwaje wakati baba alikuwa hai?

* Nini ambacho labda kilikuwa kibaya kabisa kwa mwanamke huyu wakati mme wake alikufa?

3. Je kuna shida gani za kifedha na kiakili zingeweza kutokea wakati mama analea motto wake wa pekee mwenyewe?

4. Je huyu mama alikuwa anafikiria nini juu ya Mungu alipokuwa anatembea nyuma ya cheneza la mnae?

5. Kipindi ambacho Yule kijana alikufa Yesu alikuwa katika mji wa Kapernaumu mji ambao ulikuwa umbali wa kilometa 40 kutoka Naini (7:1). Mazishi yalifanyika si zaidi ya siku iliyofwata. Kwa nini Yesu alitaka kufika katika mazishi yale mapema, hata kama ilimaanisha kutembea kwa haraka katika umbali mrefu?

* Kwa nini Yesu alitaka kumzaidia mjane huyu hata kama hakuomba msaada wake?

6. Ni katika hali gani ambayo umejisikia kuwa msaada wa Mungu husingaliweza kukufikia mapema?

*Tunawezaje kuwa na uhakika kuwa msaada wa Yesu hauchelewi?

7. Kwa nini Yesu alimwambia yule mama mwenye kulia: "Usilie!"?

* Yesu anakwambia wewe pia: "Usilie!" Je anamaanisha nini kusema hivyo?

8. Je Yesu alimfufuaje Yule kijan kutoka kwa wafu?

9. Luka anamaanisha nini anaposema: "Yesu akampa mama yake" (15)?

* Je unafikira tukio hili lilibadilishaje uhusiano katika ya mama na kijana wake?

10. Baba wa mbinguni pia alimwona mwanae wa pekee akibebwa kwweleka kaburini. Je unafikiria uchungu wake ulikuwa mkubwa kuliko ule ule yule mjane?

* Katika mstari wa 16 unasema: "Mungu amewaangalia watu wake." Kwa nini hakumzaidia mwanae alipokuwa anakufa?

# 12. MWANAMKE ALIYE SAMAHEWA MENGI Luka 7:36-50

KUMBUKA: Katika utamaduni huu, mwanamke hakutakikana kuonyesha nywele yake hadharani. Mstari wa 44-46 inasimulia jinsi wageni waheshimiwa walikaribishwa nyumbani.

1. Je Mfarisayo Simioni alifikiri nini juu ya Yesu ambaye alimkaribisha nyumani kwake (36, 39, 44-46)?

* Je unafikiri kwa nini Simioni alikaribisha nyumbani kwake hivyo?

2. Kila mtu alimfahamu huyu huyu mwanamke kwa sababu alikuwa kahama wa Mjini (37). Ebu jaribu kufikiria juu ya mwanamke huyu alipokuwa anakuwa- Ni nini labda kilimfanya awe kahaba? Fikiria juu ya wezekano mbali mbali.

* Je mwanamke huyu alikuwa na uzoefu gani kuhusu kupendwa?

3. Chupa ya marimari iliyojaa marhamu ilikuwa ghali sana. Fikiria sababu mbalimbali kwa nini huyu mwanamke aliweka akiba hela na akanunua chupa ya marimari?

4. Kwa nini huyu mwanamke alitaka kukutana na Yesu kwa kwa hali na mali? Bila shaka likuwa na ufahamu kuwa asingalipata makaribisho yoyote katika nyumba ya Mfarisayo!

* Ni nini kilimfanya mwanamke kuamini kuwa Yesu asingalimkataa?

5. Kwa nini huyu mwanamke alitaka kumgusa Yesu?

* Nini kitafanyika kama tutaguzwa na mtu Fulani au kitu ambacho hatupendi?

* Nini kilitendeka Yule mwanamke alipomgusa Yesu?

6. Ni nini kilimfanya mwanamke alie sana hadi miguu ya Yesu ikaloana?

7. Je unafikiri ni nini kilikucha kwanza hasa katika hali ya huyu mwanamke: imani yake katika Yesus au upendo wake kwake? Toa sababu zako kutokana na somo hili.

* Kama wakati Fulani ulisikia kuwa ulimpenda Yesus kwa moyo wako wote, ni katika tukio gani?

8. Katika mistari ya 41-42 Yesu anatoa mfano wa mkopeshaji. (Dinari mia tano ni sawa sawa na mshahara wa mwaka mmoja na nusu. Dinari hamsini ni sawa sawa na mashahara wa mwezi mmoja.) Dhamni inafaninishwa na deni.. Je Yesu alitaka kumfundisha Simioni kwa mfano huu?

* Ni dhambi gani za Simioni ambazo Yesu anamaanisha katika mfano huu?

9. Je ni nini kilitendeka na deni la dhambi ambalo mwanamke alikuwa nayo alimdeni Mungu?

* Ni nini kilitendeka na deni la dhambi ambalo Simioni alikuwa nayo kwa Mungu?

* Kwa nini Simioni hakumpenda Yesu?

10. Yesu ambaye anajua kabisa dhmabi zako zote, anasema kwako sasa maneno ambayo yameandikwa katiika mstari wa 48 na 50. Utamjibu nini?

# 13. MFANO WA MPANDAJI     Luka 8:4-15

KUMBUKA KWAMBA: Mfano wa mpandaji ulikuwa ni mfano wa kwanza wa Yesu, ni ajenda yake ya miaka mitatu ya huduma yaake ya hadhara.

1. Kwa nini Yesu alilinganisha neon la Mungu na mbnegu? tafuta mfanano uwezavyo.

* Je Yesu alitaka kusema nini juu ya ujio wa huduma yake kupitia kwa mfano huu?

2. Ni kwa njia gani tabithi ibilisi anaweza kuchukua neon la Mungu kutoma mioyo yetu (5,12)?

* Je tunawezaje kuzuia kitu hicho ambacho kimezungumziwa katika msatari wa 12 kutotendeka kwetu?

3. Tazama mstari wa 6 na 13. Ni jaribu aina gani linaweza kusababisha mtu kuanguka kutoka imani ya Kikristo?

* Je watu hawa katika mstari wa  13 walifurahi juu ya nini kwanza?

* Je Yesus anamaanisha nini kwa Mksriato ambaye hana “mizizi"?

4. Je “mahangahiko ya maisha, utajiri na anasa” yanawezaje kusonga neno la Mungu katika maisha yetus (7,14)?

* Kwa nini utajiri ni shida kubwa kwa Mkristo kuliko umasikini?

* Tunaweza kufanya nini tukigundua kuwa mahangahiko, utajiri and anasa vinaweza pole pole vinaweza kututenganisha na neon la Mungu?

5. Je  udongo mbya unawezaje kuwa udongo mzuri (8,15)?

* Ni katika hali gani ambayo maisha ya mwanadamu yanaweza kuzaa matunda?

6. Ni udongo gani kati ya hizo nne ambayo unafaa hasa hali ya moyo wako kwa sasa? (Jibu katika moyo wako.)

7. Je Yesu anamaanisha nini kwa kuzaa moja kwa mia kwa mimea (8)?

* Kwa nini Wakristo wengi siku hizi hutarajia “Mimea”  katika maisha yao kukua ghafula?

8. Mfano huu unatufundisha nini juu ya uinjilisti?

* Je somo hili ninafundisha nini juua ya “ nuvu ya uinjilisti"? (Kama hujui neon hili unaweza kuruka swali hili.)

9. Katika Biblia, Yesu ni sawa na neon la Mungu In the Bible, Jesus is equal to the Word of God (Kiongozi anaweza kusoma Yohana 1:1). Kuna kufanana gani kati ya Yesu na mbegu?

HABARI NJEMA: Yesu aliwambiwa wanafunzi wake usiku wa mwisho hapa duniani: Naye Yesu akawajibu, akasema, Saa imefika atukuzwe Mwana wa Adamu. 24Amin, amin, nawaambia,

Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi. 25Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele. 26Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu. Sasa roho yangu imefadhaika; nami nisemeje? Baba, uniokoe katika saa hii? Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii. 28Baba, ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni, Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena. 29Basi mkutano uliosimama karibu wakasikia, walisema ya kwamba kumekuwa ngurumo; wengine walisema, Malaika amesema naye. 30Yesu akajibu, akasema, Sauti hiyo haikuwako kwa ajili yangu, bali kwa ajili yenu. 31Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. 32Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu. 33Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa." (Yohana 12:23-33). Vivyo hivyo, mbegu katika mfano huu si kitu kingine ila neon la msalaba.

## 14. NITAKUFUATA Luka 9:57-62

1. Kuna watu watatu katika somo hili ambao wanahesabu gharama ya kumfuata Yesu. Ni katika hali gani umefanya vile vile?

2. Ni kwa nini Yesu hkumwambia mtu wa kwanza: “karibu katika kikundi changu!" (57-58)?

* Je Yesu alitaka kusema nini kwa huyu mtu aliyekuwa na jibu katika mst 58?

3. Ungefanya nini kama kitu cha kipekee ambacho Yesu alikuahidi ni maisha yanayoonyeshwa katika mstarari wa 58?

* Kwa Yesu alihitajika kushi maisha ambayo yanaoneshwa katika mstari wa 58 japo alikuwa mwana wa Mungu ?

4. Je mtu wa pili alikuwa na litoa lipi kipaombele (59-60)?

* Ebu linganisha na alilolipa kipao mbele na lile la kwako.

* Ni nini ambacho ungependa watoto wachagu watoe kibao mbele katika hali kama hii?

5. Je kifo cha mtu mmoja katika familia yetu kinawezaje kutufunga kwamba tunafikiri kuwa hatuwezi kumfuata Yesu?

6. Sababu ilikuwa nini hasa iliyosababisha mtu wa tatu kutembelea nyumbani kwake mra moja tena (61-62)?

* Kwa nini Yesu hakutaka kumkubalia faraja hii ndogo?

7. Je unafirikiria maisha ya hawa watu watatu yangekuwaje kama ingalitokea kuwa waliamua kubaki nyuma? Na kama wangechagua kuutangaza ufalme wa Mungu?

8. Katika tamaduni nyingi, pamoja na zile za siku za Yesu, mtu kuonyesha heshima kwa wazazi wake ni kitu cha maana kwa motto wa kiume kufanya. Kwa nini Yesu hapa anaenda kinyume na utamaduni wake?

* Yesu pia alifundisha umuhimu wa mtu kuwaheshimu baba na mama yake.Jesus also taught the importance of honoring one's father and mother. Je tunawezaje kuanisha somo hili na amri hii?

9. Je unafikiri kuwa vijana katika Makanisa yetu wanaonywa juu ya shida ya kumfuata Yesu akam vile Yesu aliwaonya hawa watatu?

10. Utafanya nini kama utagundua kuwa hufai kutumika katika ufalme wa Mungu?

HABARI NJEMA: Yesu alikuwa njiani kwenda Yerusalemu alipokuwa anaongea haya. Hakuangalia nyumba baada ya kuweka mkono wake katika kulima, lakini akatembea imara kuelea mateso na kifo. Alifaa ufalm wa Mungu–pengine ni yeye pekee ambaye aliwahi kufaa.. Alifaa si kwa ajili yake mwenyewe bali kwa ajili yetu.

## 15. JINA MBINGUNI Luka 10:17-20

TAZAMA: Kwa taarifa ya msingi, soma mstari wa.1 na 9. Mstari huu unazungumza juu ya hali ya maana sana halio ya uamsho wa Galilaya – Je itachukua mwendo gani? Kwa ajili ya swali ya 9* tazama Mwanzo .3:15.

1. Je unafikiri kutatendeka nini kama watu katika Makanisa yetu walikuwa na nguvu kama ya hawa 70 walikuwa nayo?

* Kwa nini hawa 70 walitoa taarifa moja hasa ya huduma yao kwa Yesu?

2. Kwa nini watu wanafurahia mamlaka na uwezo?

* Wanafunzi wake walifurahi juu ya mafanikio yao, kwa nini Yesu hakufurahi pamoja nao?

3. Kuna tofauti gani kati ya furaha juu ya huduma na furaha juu ya jina lake kuandika katika kitabu cha mbinguni?

* Kwa nini ni rahisi kufurahia juu ya vitu vya dunia kuliko mambo ya mbinguni?

4. Je wanafunzi walihubiri kwa wale ambao wanafurahi juu ya kutoa mapepo?

* Je wanafunzi wanafundisha nini juu ya wale ambao wanafurahi juu ya majina yao kuandikwa mbinguni?

5. Je nini kifanyike ili kujifunza kufrahia juu ya majina yetu kuandikwa mbinguni?

6. Ni lini na jinsi gani majina yetu yanawezaje kuandikwa mbinguni?

7. Ni lini na ni wapi umesikia mambo kama hayo yalitotajwa katika mstari 19 yametendeka?

* Ni katika hali gani unaweza kuwa na ujasiri kukanyaga nyoka na ngeu?

8. Kwa nini kitu chochote au mtu yeyote hawezi kudhuru wanafunzi wa Yesu (19)?

* Je nini ambaco unaogopa kinaweza kudhuru wapendwa wako?

* Kulingana na somo hili, ni mambo gani ambayo hatuhitaji kuogopa?

* Ni mambo gani ambayo tunahitaji kuogopa?

9. Japo wengi wa wanafunzi wa Yesu walifia dini, ni jinsi gani ni wazi kuwa walishinda nguvu za adui?

* Ni kwa nini Yule nyoka wa zamani (Ibilisi) alikubaliwa kupiga kisigino cha Yesu juu ya msalaba?

10. Je somo hili linasema nini juu ya huduma yetu?

* Je somo hili linasema nini juu ya "Nguvu ya uinjilisti"? (Kama hujui neno hilo unaweza kuacha kujibu swali.)

HABARI NJEMA: Biblia inatuambia kuwa wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima mbinguni: "  Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto. " (Rev.20:15). Kwa sababu Yesu hakutaka litendeke kwetu aliomba kama Musa alivyofanya: " Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao – na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika.  " (Kutoka.32:32).

# 16. MSAMARIA MWEMA Luka 10:25-37

KUMBUKA: Wayahudi katika wakati wa Yesu walichukia Wasamaria kwa kuwa walikuwa na damu iliyochanganywa na nusu wapagani. Wasamaria walikuwa na hekalu lao katika mlima wa .Gerizim, yapata umbali wa kilometa 50 kaskazini mwa Yerusalemu. Walitumia Mwanzo-Kumbukumbu la Torati (Vitabu vitano vya Musa) kama Biblia yao. Mtu huyu aliyejeruhiswa inawezekana alikuwa Myahudi. Kuhani na Mlawi pengine walikuwa wanaelekea hakaluni ili kuwa kutunza huduma za za kidini kule. Kama awangeguza damu wangekuwa wachafu siku nzima na hawakukubaliwa kuingia hakaluni.

1.Ebu fikiria huyu mtu aliyejeruhiwa alikuwa na mawazo gani katika kichwa chake saa baada ya saa akiwa amelala kando ya bara bara.

* Fikiria juu ya hisia za mke na watoto wakati baba alikosa kurudi nyumbani baada ya safari yake.

2. Kwa nini hawa watumisho wawili Kuhani na Mlawi hakuweza kuzaidia hutu mtu aliyekuwa mahututi wa kidini? Fikiria sababu nyingi uwezavyo.

* Je wataalamu wa sheria alifafanunuaje tabia za Kuhani na Mlawi katika mfano huu (25-27)?

3. Je Makuhani na Walawi walitafsirje amri ya Upendo, ambayo walifahamau fema kutoka Biblia zao? (Tazama mst vs. 27.)

* Kulingana na maoni yako je inawezekana kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, moyo, nguvu na mara hiyo kumtenda mtu ambaye anatezeka jinsi hawa viongozi wa dini walivyofanya? Toa sababu.

4. Msamaria alikuwa sababu nyingi kutokuzaidia aliyejeruhiwa. Fikiria sababu nyingi uwezavyo.

* Je ni msaada kiasi gani mtu mwema anaweza kuzaidia katika hali hii?

* Je ni "msaada gani zaidi" Je Msamaria alitoa kwa aliyejeruhiswa?

5. Dinari mbili ni sawa sawa na mshahara wa siku mbili, ambayo inaweza kutosha kumweka mtu hadi miezi miwili katika nyumba ya wageni. Je kiasi hicho kinaweza kuwa kiasi gani katika hela yetu?

* Kwa nini msamarai alilipa kiasi hicho kuzaidia mgeni ambaye hakuwa hata hakuwa mwanchi mwenzake?

* Je ni nani unaweza kuwa tayari kufanya chochote kama vile huru Msamaria alimfanyia huyu mgeni?

6. Je unafikiri Msamaria alitunza Amri ya kwanza ya Upendo (27)? Toa sababu zako.

7. Jirani yako ni nani ambaye pengine hajamjali kama vile Kuhani na Mlawi hawakujali mtu aliyejeruhiwa (37)?

* Ni hatua gani dhbithi ungechukua kumzaidia jiarani?

8. Kuna kufanana gani kati ya Yesu na Msamaria Mwema?

* Je Yesu alifanya nini kwa adui zake kuliko Msamaria?

* Je Yesu ametufanyia nini sisi ambao tumejisikia kuwa tumejeruhiwa katika moyo na nafsia?

(9. Jadiri mifano halisi kwa mfano kwa nini Wakristo wengi Ulaya hawakufanya chochote kuwazaidia Wayahudi ambao walijeruhiwa katika vita vya pili vya dunia. Tafuta mfano kutoka historia ya Nchi/Kanisa lako: Utumwa, buraku-mondai n.k)

## 17. KITU CHA PEKEE KINACHOHITAJIKA   Luka 10:38-42

KUMBUKA: Nafasi ya wanawake haikuwa sawa wakati wa Yesu kama ilivyo sasa. Pamoja na vitu mambo mengine , wanawake wasingalisoma Biblia pamoja na wanaume.

1. Je unategemea nini kutoka kwa zaidi kutoka kwa kumtembelea rafiki mzuri?

* Yesu na wanafunzi wake walikuwa nje siku nzima. Je unafikiri walitegemea nini kutokana na kukaa kwao katika nyumba ya dada hawa wawili?

2. Ebu fikiri juu ya hisia za Martha na Mariamu kuzulu kwa Yesu.  Ni lipi raisin a kwa nini ni raisi kuelewa na kwa nini?

3. Tunaweza kuona shida ya Martha katika mstari wa 40. Ilikuwa nini?

* Nini kilimfanya Martha kufadhaishwa na Yesus na wala si dada yake tu?

* Ni katika hali gani unaweza kusema kwa Yesu: "Bwana, huoni vibaya...?"

4. Je Mariamu alifikiri juu ya chakula cha jioni?

* Kwa nini Yesu angalitaka mariamu pia kusikiliza mafundisho yake?

5. Dhambi ya wakristo wana moyo wa kumtumikia Yesu kuliko musikiliza sauti yake. Kwa nini?

* Inaonyesha nini juu uhusiano kati ya watu wawili kama mmoja kati yao hana moyo wa kusikiliza mwingine anachotaka kusema?

6. Yesu ana maanisha nini kwa; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu " (42)?

* Je unakubaliana kuwa kumsikiliza Yesu ndicho kitu cha pekee ambacho unahitaji maishani na kifo?

7. Kwa nini Yesu anataka usikilize neon lake muda wote?

* Nini kitatendeka kwetu kama tukimsikiliza Yesu kwa kipindi fulani?

* Wapi na jinsi gani tunaweza kusikiliza maneno ya Yesu siku hizi?

8. Tukiamua kufanya jambo fulani, ina maana kuwa tuna amua kuacha jambo linguine katikati ili tupate nafasi kuseoma Biblia and kwenda katika mikutano ya Kikristo?

9. Ni nani unafikiri Yesu alipenda zaidi, Martha au Mairmu?

* Ni mstari gani katika hii mistari unafikiri Yesus anakuzugumzai wewe leo: mstari wa 41 au 42?

10. Kitu kinachohitajika katika maisha haya na kifo ni kusikiliza neon la Mungu. Kwa Yesu hakuyasikiliza alipokuangikwa msalabani?

## 18. SAMAKI AU NYOKA? Luka 11:5-13

1. Yesu anataka kufundiaha juu ya maombi kupitia kwa mfano huu mdogo katika somo hili. Je unapa kufanana gani unapata katika hali yako ile ya Yule mwanaume katika mfano huu?

* Ni katika hali gani umedai katika maombi yako kama vile huyu mwanaume katika mfano huu?

2. Rafiki ndani ya nyumba anaonekana kutokubali kufanya kama anavyo ulizwa. Kwa nini Yesu anamfananisha Mungu kama "Rafiki" hivyo?

3. Ni nini kilichomfanya mtu wa kwanza kusisitiza hadi apipotpata alichokitaka?

* Tunaweza kupata wapi uvumilivu katika kuomba hadi Mungu atakapo jibu maombi yetu?

4. Fundisho juu ya maombi yetu anatumia tenzi mbalimbali: kuomba, kutafuta, na kupisha (9-10). Ni kipengele gani katika maisha ya maombi yetu vitenzi hivi vinaelezea?

* Mda huu kuna kitu gani ambacho umeomba ili upate, unatafuta na kupisha ili upokee? (Jibu moyoni mwako.)

5. Intufundisha nini Yesu anapofananisha na motto kuomba kitu kutoka kwa baba yake?

* NI kwa njia gani baba yetu wa mbinguni anafanana na Yule baba yetu wa hapa duniani ?

6. Nini baba ambaye mwenye upendo anafanya kwa mtoto wake kama anajua kuwa kitu anacho kiomba si kitu kizuri kwake?

* Tutajuaje kama tunacho kiomba kwa ajili ya wapendwa wetu ni kizuri kwao na kwetu pia?

7. Je umewahi kupata kuwa kitu mabacho ulifikiri kwanza ni "nyoka" umegeuka baadaye kuwa "samaki" (or au labda kinyume chake)? Tusimulie.

8. Ni nini ambacho ni muhimu kwako: Kwamba Mungu anaweza kujibu maombi yako sasa au anaweza kujibu katika ulimwengu mpya na mbingu mpya? Toa sababu.

9. "Tazama, mkono wa BWANA haukupunguka, hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; 2lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia." (Is.59:1-2). Fikiria juu ya mistari hii kabla hujajibu swali lifwatalo: Kwa nini Mungu hakusikia sauti ya mwanae alipoomba msalabani.?

## 19. TAJIRI MPUMBAVU Luka 12:13-21

1. Unafikiri ni kwa nini kuna kugombana juu ya urithi kumekuwa kitu cha kawaida hata katika familia nzuri?

* Kuna tofauti gani kati ya huyu mtu katika mstari wa 13 na watu wengine katika injili ambao walimwomba Yesu awazaidie?

2. Shida ya huyu mwanaume katika mstari wa 13 ilikuwa nini hasa?

* Kungetokea nini kama Yesu angalifanya kama huyu mtu alivyomwomba?

3. Tazama sasa mfano katika mstari was 16-20. Fikiria maisha ambayo huyu tajiri alikuwa ameishi. Je yalikuwa maisha ya furaha au sio? Toa sababu zako

* Je ungependa watoto wako waishi maisha ambayo shida ambayo wangekuwa imetajwa katika mstari wa 17?

4. Kwa nini Mungu anatoa jua na mvua kwa mashamba ya mtu ambaye hajawahi kumshurkuru hata mara moja kwavyo?

* Je dini (mungu) ya huyu mtu tajiri ilikuwa nini?

5. Je tunajifunza nini juu ya uhusiano wa kibinadamu wa huyu mtu tajiri?

* Je kosa nini kosa kubwa la huyu mtu?

6. Tumia mfano huu katika nchi tajiri na masikini. Ni dhambi gani zetu ambazo Yesu anamulika kupitia kwa mfano huu?

* Je unahitaji kutumia vipi pesa na mali uliyo nayo?

7. Kwa nini huyu mtu tajiri hakutambua kuwa angekufa kabla hajachelewa?

* Ni katika hali gani unafikiri juu ya kifo chako na hukumu inayokuja?

8. Je mstari wa 21 una maanisha nini? (Je huyu mtu tajiri angewekaje hazina yake mbiguni? Je kuwa tajiri mbele za Mungu kuna inamaana gani ?)

9. Linganisha tajiri mpumbavu na Yesu – kuna tofauti zipi ?

* Kwa Mungu alihitisha uhai wa Yesu, vile anavyo udai kutoka mtu tajiri (20)?

* Ni nani alifaidi kutokana nayale Yesu alipokea akiwa duniani (20b)?

# 20. MWAMINIFU NA SIYE MWAMINIFU Luka 12:35-48

KUMBUKA: Neno "Mtumishi" pia inamaanisha "mtumwa".

**Mistari ya 35-40**

1. Mtumishi anahitaji kufanya nini aweze kuwa macho usiku wote?

* Ni nini kitatendeka kama mtumishi akilala kabla bwana wake hajarudi?

2. Je unafikiri ni raisi kusubiri kwa kurudi kwa kurudi kwa Yesu mara ya pili? Kwa nini au kwa nini sio?

* Kwa nini kurudi kwake Yesu kumefananishwa na mwizi anayevunja na kuingia katika nyumba?

3. Ni nini ambacho Yesu anakuhadharisha dhidi yake katika mistari ya (35-40)?

* Unawezaje katika katika utendeji, kumfungulia Yesu mlango leo?

**Mistari ya 41-46**

4. Linganisha hawa watumishi wawili katika mistari hii, mwema na mbaya. Kuna tofauti zipi?

* NI nini kunacho wafanya hawa mawakili wawili kutenda njia tofauti?

5. Linganisha uhusiano wa hawa mawakili wawili na bwana wao? Ni nini kinacho tofautiano kati yao?

* Je hali yetu juu ya kurudi kwake Yesu ina hadhirije huduma yetu katika huduma katika ufalme wa Mungu?

6. Ni mambo gani ambayo Yesu alikabidhi kwa “mawakili” wa kanisa lake hadi atakaporudi?

* Ni huduma gani ambayo Yesu amekukabidhi wewe ninafsi?

7. Ni wapi tunawakuta hawa “mawakili” wa Kanisa ambao wanawapiga watumishi wenzao, kula na kulewa?

* Ni adhabu gani inayowasubiri hawa “mawakili”?

**Mistari ya 47-48**

8. Ni kosa la nani kwamba kuna watu katika dini ya Kikristo ambao hawajui mapenzi ya bwana wako?

* Ni kwa kipimo gani ambacho watumishi wa Mungu watahukumiwa mwishowe?

**Muhtasari:**

9. Ni linin a ni wapi Yesu anajifunga ili tutumikia and kuja kutusubiri (37b)?

10. Kwa nini Yesu alihitaji kuzoea hatima ya mtumishi asiye mwaminifu: Aliwekwa katika mahali pa wasio amini na kuongea, kukata vipande vipade (46b)?

## 21. MKUYU TASA Luka 13:6-9

KUMBUKA: Mfano huu unazungumza juu ya Israeli. Kwa mda wa miaka mitatu Yesu alijihuzisha katika na taifa hili bila kupata matunda yakutosha katika taifa hili. Mfano huu hata hivyo unazungumza juu yetu pia. Wewe ndiye mkuyu, Mungu ndiye mmliki wako na Yesu nidye anaye tunza mti. Ujumbe nyuma ya mfano huu unaweza kuangalia pia katika Mathayo 21:18-19.

1. Udongo katika shamba ulikuwa udongo bora kabisa. Je Yesu alitaka kusema nini juu ya Israeli kwa kuweka mkuyu miongoni mwa misabibu?

* Je huyu Mkuyu tasa ulileta madhara gani kwa misabibu iliyo uzunguka?

2. Je ni matunda ya aina gani labda Mungu alitarajia kutoka maishani mwako kwa miaka mitato iliyopita? (Jibu maishani mwako.)

* Ni sababu gani ahsa zinazokuzuia kuzaa matunda kwa ufalme wa Mungu?

3. Je mtunzaji wa misabibu alikuwa na hisia gani dhidi ya mkuyu tasa?

* Kwa nini Yesu anawapenda Wakristo hata wale ambao hawazai matunda yoyote?

4. Ebu fikiria Yesu amesimama mbele za Baba yake akiomba nyongeza ya mda kwa ajili yako. Ni nini kunamfanya afanye hivyo?

5. Mtuzaji wa misabibu ana ahidi kupalilia kuutilia samadi. Je Yesu amefanya nini maishani mwako kwa mka wa miaka mitatu iliyopita ili kukuwezesha kuzaa matunda kwa baba yake wa mbinguni?

* Je ni jinsi gani kukata tama na mateso katika maisha yetu vinachangia katika kuzaa matunda?

6. Kulingana na mfano huu, kitatendeka kwa Mkristo ambaye mwishowe hatazaa matunda?

7. Geukia Mathayo 21:18-19. (Kingozi asome mistari hii.) Tukio hili lilitokea katika juma la mwisho la maisha ya Yesu. Fikiria sababu mbalimbali kwa nini Yesu alitaka kuulaani mkuyu tasa?

* Mistari hii miwili ina uhusiano gani na kifo cha Yesu.

HABARI NJEMA: Baada ya kulaani mkuyu tasa, Yesu alichukua nafasi yake – Nafasi ya Israel, nafasi yako na yangu. "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti." (Wagalatia 3:13).

# 22. MWANA MKE MWENYE NUNDU Luka 13:10-17

KUMBUKA: Hekalu palikuwa ni mahali ambapo watu walikusanyika kila Jumamosi kusikiliza neno la Mungu. Wanawake hakuwa na sauti katika mambo yanayohusu dini wakati hule; walikaa au kusimama barazani au katika vitu vya nyuma. Hatujui nini kilikuwa shida katika mogongo wa huyu mwanamke, lakini pengine alikuwa na nundu.

1. Ebu fikiria maisha ya kila siku ya huyu mwanamke kwa kipindi cha miaka 18 ya ulevamvu wake.

* Je unafikiri watu walimtendeaje huyu mwanamke mwenye nundu (14)?

2 Kama ungelemaa wakati wa ujana wako, je unafikiri ni kitu gani ambacho kingalikuwa kigumu kwako?

* Kama ungalilemaa wakati bado ukiwa kijana wako je ungefikiri nini juu ya Mungu ambaye alikubali litendeke?

3. Yesu aliposhughulika na walio kupakawa na pepo alizungumza na peopo moja kwa moja. Katika somo hili hakufnya hivyo kumaanisha kuwa huyu mwanamke hakupawa. Je Yesu anamaanisha nini anaposema kuwa ni Shetani aliyemfunga (16)?

* Ni vitu gani ambavyo vinaweza kutufunga sisi watu ili kwamba hatuwezi kuishia maisha kamili?

4. Huyu mwanamke hakuja Hekaluni ili kuponywa. Alikuja kufanya nini?

* Ilimaanisha nini kwa huyu mwanamke kusikiliza neon la Mungu mara moja kwa Juma?

5. Kwa nini huyu mwanamke hakumwomba Yesu msaada? Fikiria sababu mbalimbali.

* Je unafikiri alijisikiaje wakati Yesu alimwita kuja mbele na has mbele ya watu wote?

* Ni nini kilichomfanya afanye kama vile Yesus alimwomba kufanya?

6. Kulingana na kifungu hiki, ni nini kinachowazaidia watu ambao kwa njia moja au nyingine wamefungwa na Shetani? (Singatia kifungu!)

7. Yesu anamaanisha nini anapomwita Yule mwanamke “uzao wa Ibrahimu? Fikiria uwezekano mbalimbali. (Kwa Ibrahimu "? ( tazama muhtasari katika somo la #28.)

8. Je mtazamo wa Yesu kwa Yule mwanamke unatofautianaje na wa Yule mkuu ya Hekalu?

* Mkuu wa Hekalu alifikiri kuwa alimwamini Mungu. Je ni nini kilikosa katika imani yake?

* Ni nini kilichomfunga yule mkuu wa?

HABARI NJEMA: Shetani mwishowe alimfunga Yesu mwenyewe- kwa misumari msalabani. Hii ndio sababau sasa anaweza kuwafungua kutoka vifungo vya shetani wote ambao wanaotaka kuwa huru.

# 23. MLANGO ULIO MWEMBAMBA      Luka 13:22-30

1. Je unafikiri ni kwa nini mtu Fulani angependa kujua jibu la Swahili hili raisi lililo katika mstari wa.23?

* Kwa nini Yesu hakujibu swali hili kwa njia rahisi tu, ndio au hapana?

2. Ni kwa njia gani mlango wa mbinguni ni mwembamba?

* Ni kwa watu wa aigna gani mlango wa ufalem wa mbinguni ni mwembaba hasa?

3. Ni kwa njia gani watu wanajitahidi kuingia katika mlango mwembamba (24)?

4. Kufuatana na haya Yesu anasimulia mfano mdogo kuhusu karamu katika ufalme wa Mungu (25-27). Je Yesu anataka kusema nini kwa wasikilizaji wake kupitia kwa mfano?

5. Kwa nini watu katika mfano huu hawakuweza kupitia mlango mwembamba wakati walikuwa na wakati?

* Je mfano huu unahusianaje na swali katika mstari wa vs.23?

6 Je Yesu ana maanisha nini anaposema kuwa hawajui watu ambao walikula na kunywa pamoja naye ambao pia walisikia mafundisho yake?

* Je tunawezaje kujua kuwa Yesu atatufahamu siku ya mwisho?

7. Mababu wa imani ambao wanatajwa katika msatari wa 28 walikuwa na madhaifu yao na dhambi. NI nini kilichowawezesha kuingia kupitia mralango mwembamba kuingia katika ufalme wa Mungu? (Jadili lingana nay ale ambayo unakumbuka juu mababu wa imani- usijaribu kusoma haya sasa.)

* Ni nani wengine ambao watafika katika karamu ya ufalme wa Mungu (29)?

8. (Kiongozi asome Yohana 10:9.) Je ufalme mwafundisho ya Yesu kuhusu mlango wa mbinguni yanatofautianaje katika sehemu hizi zingine mbili?

* Kwa nini mlango mmoja ni mwembamaba na mwingi ni wazi kwa mtu yeyote?

HABARI NJEMA: Ni vigumu kwa mwenye dhambi kuokolewa kupitia kwa malango wa sheria sawa sawa na vile ngamia kupitia katika tundu la sindano (Mathayo.19:24). Ni Yes utu ambaye aliweza kupitia mlango wa sheria. Mlango wa njili ni wazi kwa kila mtu kwa sababu ni mlango ambao dhambi husamahewa.

## 24. MFANO WA KARAMU KUU        Luka 14:12-24

KUMBUKA: Wageni ambao waliopokea mwaliko wa kwanza walikuwa ni Wayahudi. Sasa tunaweza kutumia mistari ya 16-20 kwa wote ambao wameitwa na Mungu kupitia kwa upatiso na neon la Mungu.

1. Kumbuka mara ya mwisho ulipokuwa na sherehe. Je ungefanya nini kama mtu angali kuambia ufanye kilingana na mstari wa 12-14?

* Kwa nini Yesu anatwambia tuwaalike masikini na wagonjwa katika sherehe zetu?

2. Tazama mistari ya 18-20. Sababu ilikuwa nini hasa kwa nini hawa watu watatu walikataa kuingia katika karamu?

* Kwa nini mara nyingi tufikiria juu ya tulivyo navyo (18), kazi zetu (19), na maisha yetu ya ndoa (20) kuwa muhimu zaidi kuliko ufalme wa mbinguni?

* Ni sababu gani hizi tatu unaguza maisha yako? (Jibu moyoni mwako.)

3. Ni katika kiwango gani waalikwa walimtambua? Mmoja wapo ya tafsiri ni, kwamba walioalikwa walikataa mwaliko kwa sababu walijua kwamba wasingaliweza kulipa deni katika siku za usoni (12b) Kama hili ni kweli inasema nini juu ya wale waliokataa kufika?

* Ni kosa gani kubwa wale ambao walikataa kufika walifanya?

4. Karamu katika mfano huu ina maanisha mbinguni. Kwa nini watu wengi hawataki kwenda huko?

5. Kuna tofauti gani kati ya wale ambao walialikwa kwanza na wale ambao miwshowe walifika katika karamu?

* Kwa nini kundi la pili lilikubali mwaliko hata kama wale walioalikwa kwanza hawakuweza?

6. NI akina nani ambao ni “maskini, na vilema, na vipofu, na viwete” –Wale ambao wanakubali kwa furaha mwaliko kwenda mbinguni (21)?

* Kwa nini hawa watu hawakujali juu ya kuwaalika pia ili kuwali waliowaalika kwanza?

7. Je mstari huu wa 23 unamaanisha nani?

* Je mstari huu unatufundisha nini juu ya uinjilisti (Kutangaza Injili)?

8. Je unaegemea upande gani katika makundi haya? (Jibu katika moyo wako.)

* Je Mungu amefany nini katika moyo wako ili kuweza kukuhamisha kutoka kundi ili mbalo linakataa mwaliko katika kundi ambalo linakubali ?

9. " Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari!" (17) Je Yesu aliweza kulipa nini ili aweze kukupa karamu hii?

* Yesu anasema katika maneno haya: "Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari!" Jibu lako ni nini?

HABARI NJEMA: Yesu alifanyika masikini "maskini, vilema, viwete, vipofu" ili kuweza kulipia karamu mbinguni. Hii ndio sababu mwaliko sasa ni bila malipo kwa kila mtu ambaye anataka kuja.

## 25. Kondoo Aliyepotea  Luka 15:1-7

1. Fikiria sababu zingine kwa nini watosha ushuru na wenye dhambi wengine walipotea mbali zaidi ya kufikia sauti ya Mungu (1).

* Kwa nini kila mara tunapoea mbali bila kufikia sauti ya Mungu?

2. Je kondo aliyepotea anaweza kufanyi nini ili kujizaidia ili apatikane- na je nini mbacho hawezi kufanya?

* Je mwenye dhambi anaweza kufanya nini ili Yesus aweze kumpata – na nini ambacho hawezi kufanya?

* Ni faraja gani ambayo ipo katika mfano hu kuhusu watu ambao unawasikitia?

3. Yesu ana fananisha kupatikana kwa kondo na toba. (7). Toba ni nini basi kulingana na mfano huu? (singatia somo!)

4. Je unfaikifi ni wapi tunaweza kupata hawa "watu waheshimiwa ambao hawahitaji toba" (7)?

* Kuna mstari katika kitabu cha Isaya ambacho Mafarisayo walisoma mara nyingi: **" Sisi sote kama kondoo tumepotea;Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na BWANA ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.**" (Isaya.53:6). Mara nyingine: 99 ni akina nani?

5. Ni dhambi gani ambazo Wayahudi walihitaji kutubu (2)?

* Kwa nini Wafarisayo hawakutambua kuwa walikuwa wapotevu?

* Je wewe unafikiri uko katika kundi gani: waliopotea au waliopatika?

6.Katika mifano ya Yesu, karamu humaanisha uzima wa milele mbinguni. Kwa nini sherehe ni kwa ajili ya kondoo ambayo ilipotea na si jumuisha kondoo wengine 99 (6)?

7.Inamaanisha nini kuwa hakuna yetote anayeweza kufika mbingunikwa maguu yake miwili (5)?

8. Je tunweza kumkuta Yesu ambaye anawakaribisha wenye dhambi na hata kula nao (2)?

HABARI NJEMA: Yohana mpatizaji alimfananisha Yesu na Kondoo. Alfanyika mwanakodnoo wa Mungu achukuaye dhambi ya ulimwengu (Yohana 1:29). Yesu  akam kondo hakuokolewa kutoka jangwani- badala yake, aliuawa kule. Hkubebwa nyumbani, lakini alipewa kubeba dhambi zetu zote.

# 26. MWANA MPOTEVU    Luka 15:11-24

KUMBUKA: Nyumba katika Mashariki ya Kati kwa kawaida haiwezi kusimama yenyewe mlimani ila katika sehemu ambayo ína watu wengi vijijini karibu barabrani. Sehemu ya pekee ambayo inaruhusu kuona mbali ni juu ya paa ya nyumba. Kumbuka pia kwamba wanaume wenye heshima katika Mashariki ya Kati hawawezi kukimbia.

1. Kwa nini huyu kijana hakuridhika na maisha yake nyumbani hata ingwa alikuwa na nyumba nzuri na baba mwema?

* Kama ungelikuwa katika nafasi ya baba je ungejibuje ombi la mwanao?

2. Kwa nini Mungu hajaribu kumzuia mtu ambaye anataka kuondoka?

3. Je una maoni gani juu ya maisha aliyoishia huyu kijana akiwa ngambo- alikuwa na furaha au hakuwa nayo?

* Kwa nini watu wengi siku hizi wanapenda kushi maisha ya aina hiyo- kusafiri ngambo na pesa nyingi bila kujali ya kesho?

4. Nguruwe ni mnyama ambao si msafi kulingana na Wayahudi. Je unafikiri huyu kijana alijisikiaje katika hali hii ambayo imesemwa katika mistari ya 14-16?

* Je huyu kijana alikuwa na uchanguzi gani katika hali hii?

* Je una uchaguzi gani katika hali yako ya sasa inapofika katika upande wa uhusiano wako na Mungu?

5. Mistari ya 18-19 ina toba ya dhambi ya huyu kijana. Dhambi zake zilikuwa zipi dhidi ya mbinguni? Kwa nini alikiri dhambi zake kwanza?

* Je alikuwa na dhambi gani mbele ya baba yake?

6. Ni kwa njia gani huwa tunafikiri kama mwana mpotevu: ” sistahili kuitwa mwana wa Mungu " (19)?

* Ni lini mtu ansitahili kuitwa motto wa Mungu?

7. Kwa nini kijana hakusema kwa baba yake yote aliyopanga kuyasema (18-19 na 21)?

8. Je baba alikuwa anafanya nini miaka hii yote (20)?

* Je unafikiri baba alimsamahe mwanae lini?

* Ni lini kijana alinaza kuamini katika upendo wa baba yake?

9. Je Yesu mwenyewe yuko upande gani katika mfano huu?

HABARI NJEMA: Mfano wa mwana mpotevu unatufundisha kitu juu ya Yesu kwa namna nyingine. Yesu pia aliondoka nyumbani na kutoka kwa baba yake ila kwa sababu zingine: kutimiza mapenzi ya baba yake.Na bado, aliporudi nyumbani katika mwisho wa maisha yake,hakupata makaribisho jinsi aliyopokea mwana mpotevu. Kwa kweli ilifanyika kinyume: Kwa kusema mlango ulipamishwa usoni mwake. Kwa nini?

## 27. MWANA MPOTEVU MWINGINE Luka 15:25-32

1. Kwa nini Kijana wa kwanza hakutoka nyumbani kama vile alivtofanya yule mdogo?

* Huyu mtu alitamani nini kuliko vyote?

* Kwa nini hakukua na furaha yeyote katika huyu mtoto wa kiume wa kwanza?

2. Kwa nini mtoto mvulana wa kwanza hakujihesabu kuwa mtumwa kuliko kuwa mridhi (12b, 29, 31)?

* Kwa nini huyu kaka hakuamini maneno ya babake?

3. Ni kwa njia gani umejisikia kuwa umefanya kazi ya Mungu bila kupata “hata mbuzi” kama zawadi (29)?

4. Mtoto wa kwanza alimhabisha baba yake mbele ya kijiji chote kwa kutkataa kufika katika katika karamu. Je unafikiri ni sababu gani hakumpenda baba yake?

* Jadili kwa mjibu wa mfano huu: Kama hatumpendi Mungu ni sababu gani hasa?

5. Mtoto wa kwanza alijidanganya kwa kufikiria kuwa alitimiza amri za baba (29). Ni nini mapenzi ya baba kuhusu mwanae?

* Ni kwa njia gani ahta waumini waaminifu wanaweza kwenda kinyume na Mungu bila kufahamu?

6. Katika mfano wa Yesu, karamu huashiria mbinguni. Ni nani kulinga na mfano huu anaenda mbinguni na Yule asiye?

7. Kwa nini Yesus anaonekana kuingia mfano huu ukiwa katikati (32)?

8. Ebu fikiria hali ambayo ilitenda aubuhi iliyofuata wakati hawa ndugu wawili walienda kufanya kazi shambani – je hisia zao zilitofautianaje?

9. Je Yesu mwenyewe yuko wapi katika mfano huu?

HABARI NJEMA: Yesu alikuwa na haki ya urithi sawa na Yule kijana mkubwa alivyokuwa nayo lakini aliacha haki zake. " ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." (Wafilippi 2:6-8). Kwa njia hiyo Yesu aliwaokowa watu kama vile ndugu mkubwa, ambaye wamefungwa katika utumwa wao. Yesu atawaweka huru – uwapo tu watakubali urithi wa bure.

# 28. TAJIRI NA LAZARO Luka 16:19-31

KUMBUKA: Abraham alikuwa mtu mwenye sifa kuu kwa Wayahudi na baba wa Imani kwa Wakristo. Alikuwa mtu tajiri. Jina "Lazarus" maana yake ni kwamba “Mtu ambaye Mungu anamzaidia" au kwa uraisi "Mungu anazaidia". Huu ndio mda tu ambayo Yesu alitoa jina katika mtendaji katika mifano. "Musa na Manabii" ni kufupi cha “Agano la Kale” Biblia ya wakati wa Yesu.

1. Ni vitu gani vizuri ambavyo huyu mtu tajiri alifuahia wakati wa maisha yake? Fikiria kwa wingi uwezavyo.

* Je unaweza kufikiria kitu chochote jema katika maisha ya Lazarus wakati akiwa duniani?

2. Kwa nini tajari hakumzaidia masikini Laazaro japo alimwona kila mara alipotoka nje?

* Kama mtu angetendea mototo wako kama vile tajiri alivyomtenda Lazaro, je unafikiri hukumu gani itafaa?

* Je Lazaro wa leo ni nani ambaye ungehitaji kuzaidia? (Kumbuka watu wengine wana njaa ya mambo mengine kuliko chakula.)

3. Kwa nini mtu apewe jina kama “Mungu anazaidia” kwa motto wake? Fikiria sababu mbalimbali?

* Je sababu ni hasa ambayo alitaka kumpa jina huyu masikini katika mfano wake ?

* Je Mungu alimzaidia Lazaro?

4. Kuna uwezaekano mkubwa sana kwamba Lazaro alimwomba Mungu ili ampe afya njema na liziki ya kila siku.

Angezaje kuendelea kumwamini Mungu ambaye hakujibu maombi yake jinsi alivyotaka?

* Je kama Lazaro asingali mwamini Mungu, maisha yake yangalikuwaje tofauti?

5. Lazaro alipokufa, kuna uwezekano mkubwa kwamba litupwa katika kaburi la masikini bila mazishi. "Yule tajiri naye akafa, akazikwa", maandiko yamasema (22). NI hotuba ya iana gani ambayo labda ilitolewa katika mazishi yake?

6. Kwa nini tajari alitupwa Jehanamu?

* Kwa nini Lazaro alikubaliwa mbinguni?

7. Tajiri na Ibrahamu walizungumza katika mstari wa 27-31 jinsi watu wanaweza kufahamu Mungu na wameokolewa. Je mtu tajiri alifikiri nini juu ya hili?

* Kulingana na Ibrahimu, kwa nini muujiza hauleti imani?

8. Kwa nini mtu yeyote hawezi kuokolewa bila Biblia (29-31)?

9. I kwa njia gani maisha ya Lazaro yanfanana nay ale ya Yesu? (Singatia, mateso yao na imani zao n.k.)

* Yesu alitapili nini kuhusu kufufuka kwake (31)?

10. Yesu anafundisha nini juu ya "injili ya utajiri" kupitia kwa mfano huu? (Kama hujui, unaweza kuruka swali hili.)

# 29. KUMI WAPONYWA, MMOJA KAOKOKA    Luka 17:11-19

KUMBUKA: Wakati wa Yesu, wakoma waliishi wakitenganishwa kutoka kwa watu wengine. Kama mtu alifikiri kuwa ameponywa alihitaji kujionyesha kwa makuhani (Walawi 13-14). Agano la lote linataja mara kama mara mbili au tatu tu za miujiza ya namna hiyo. Viongozi wanaweza kutazama katika ensaiklopidia juu ya ukoma. Kwa Wasamaria, Wayahudi wakiwadharau kwa kuwa walikuwa wageni na wakapagani.

1. Fikiria siku hawa watu kumi walipogundua kuwa walikuwa wamepata ukoma. NI mawazo ya aina gani yalikuwa katika akili zao kuhusu siku za maisha yao ya usoni kwao wenyewenyewe na familia zao?

(* Unaona mfanano gani kati ya ukoma na wakati wa Yesu na kupata UKIMWI leo?)

2. Je unafikiri ni mambo gani ambayo yalijitokeza katika maisha ya hawa wagonjwa ambao walitengwa?

3. Je hawa wakoma walitarajia Yesu awafanyie nini- tazama maombi yao katika mstari wa 13?

4. Mpaka kati ya Samari na Galilaya ni umbali wa 50-60 kilometa kutoka miji ambayo makuhani walikaa. Fikiria sababu mbali mbali kwa nini Yesu hakuwaponya hawa wanaume papo hapo, badala yake akawatuma mbali sana?

* Ni nini kiliwafanya hawa wanaume kuanza safari ndefu, hata ingawa hawakuwa wameponywa bado?

* Je unaweza kuwaita hawa wanaume kumi kuwa waaminio au wasio amini mara tu walipoanza safari yao?

5. Makuhani wa Wakiyahudi hawakutaka kuwa na uhusiano wowote na Wasamaria. Kwa nini Msamaria mmoja alinanza safari na hawa Wayahudi?

6. Fikiria sababu mbalimbali kwa nini hawa Wayahudi hawakuweza kurudi kwa Yesus ili kumshukuru?

* Kwa nini Msamaria alirudi kumshukuru Mungu?

7. Kwa nini alisikitishwa juu wale tisa ambao hawakurudi kwake?

* Je unafikiri umeweza kumkashirisha Yesu kwa tabia kama zile zile za hawa wanaume tisa walivyoonyesha?

8. "Imani yako imekuponya” inaweza kutafsiriwa “Imani yako imekuokoa” . Kwa nini alipenda kusema maneno haya kwa Msamaria?

9. Kuna tofauti gani kati ya Imani inayotafuta uponyaji na Imani inayotafuta Yesu mwenyewe?

* Kwa nini “Imani ya uponyaji” haiwaokoi watu waliyo nayo?

10. Je miaka ya kutengwa na aibu ilimaanisha nini kwa hawa Wayahudi tisa, wakati walifikiri juu yao baadaye?

* Je miaka ya ugonjwa ilimaanisha nini kwa Msamaria?

HABARI NJEMA: Yesus aliweza kusikia hali ya kutengwa na aibu msalabani jinsi vile wale wakoma walivyojisikia: " Alidharauliwa na kukataliwa na watu;Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko;Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. 4 Hakika ameyachukua masikitiko yetu,Amejitwika huzuni zetu;Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa,Amepigwa na Mungu, na kuteswa." (Is.53:3-4). Hiyo ndiyo gharama ambayo Yesu alilipa kwa muujiza huu.

## 30. MFANO WA MJANE    Luka 18:1-8

KUMBUKA: Wanawake wakati wa Yesu wasingaliweza kumstaki mtu wala kuwa shahidi kotini. Ndugu zao wa kike waliweza kuwazaidia wakati wa mambo ynayohusu mahakama kianiaba yao. Mjane huy bila shaka hakupata msaada wowote wa namna hiyo. Pengine ndugu zake wa kiume walijaribu kuchukua urithi kutoka kwa watoto wake.

1. Kumbuka wakati ulimlilia msaada kutoka kwa Mungu usiku na mchana. Ni kwa nini ni raisi sana kuacha kuomba wakati kama (1 na 7)?

2. Fikiria maisha ya huyu mjane. Ni shida gani alikumbana nayo alipowalea watoto wake pekee yake?

3. Ni nini kinawafanya watu sawasawa na kadhi huyu katika mfano huu: Kwamba hawamwogopi Mungu na wala kujali wanadamu (2)?

* Kwa nini Yesus alimfananisha Mungu na kadhi asiyetenda haki?

* Je umewahi kujisikia kana kwamba Mungu ni hakimu asiye mhaki? Kama umewahi ni lini?

4. Mjane aliridhika kwamba kadhi asiye asiye mhaki mwishowe atamzaidia. Kwa nini?

* Tunawezaje kuwa na uhakika kwamba Mungu mwishowe atawazaidia wapendwa wetu na sisi pia?

5. Ni nini kilifanyaki katika moyo wa huyu mjane alipokuwa analilia msaada kila wakati?

* What happens in our hearts while we are praying a long time in spite of God's silence?

6. Je maneno ya Yesu katika mstari wa 7-8 yana maana gani?

7. Yesus alisimama mble ya kadhi. Je kulikuwa na mfanano na tofauti gani katika hali hizi mbili-ile ya kwake na na ya mjane? (Usisome, jadili kutoka kumbukumbu katik akilini mwako.)

* Maombi ya Yesu yanatofautianaje nay ale ya huyu mwanamke (3)?

* Je hukumu ya Yesu ilitofautianaje na ile ya yule mjane?

* Hukumu ya Yesu ilikuwa ya haki au sio haki?

8. Mstari wa 8b unahusu nini juu ya mfano huu?

9. Mfano huu unakufundisha nini wewe binafsi juu ya maombi? (mstari wa 1, 5, 7, 8)?

HABARI NJEMA: Pilato alipomhukumu Yesu alikuwa kadhi asiye mwenye haki. Lakini Mungu alipomhukumu Yesus kufa alikuwa mhaki, kwa sababu dhambi zako na za kwangu zilihesabiwa kwake wakati ule.

## 31. NANI MWENYE HAKI? Luka 18:9-14

KUMBUKA: Mfano wa Mfarisayo na mtosha ushuru Hekaluni ni mafundisho ya msingi ya Yesu juu ya Mafundisho ya dini ya kuhesabiwa haki. Mafundisho haya yahajibu swali: Ni nani anayeweza kuwa salama na Mungu na kuweza kwenda mbinguni.? Kumbuka kwamba neon Mfarisayo havikuweza kuingia katika akili za watu kuwa wanafiki wanaojitakia haki, ila mtu ambaye anamwamini na kumwogopa Mungu kweli. Wafarisayo walikuwa upande wa masikini pia. Watosha ushuru kwa upande mwingine walikuwa wasaliti wan chi ya baba yao na waliwanyonya masikini.

1. Ni nini kinaonyesha kwamba hawa wanaume wote walimwamini Mungu?

* Kwa Wayahudi Hekaluilikuwa ni sehemu ya upatanisho na ni sehemu ambayo waliweza kukutana na Mungu. Jadili: Ni kwa sababu gani Mfarisayo katika somo letu waliweza kwenda Hekaluni?

* Kwa sababy gani huyu Mtosha Ushuru aliweza kwenda Hekaluni?

2. Mfarisayo walishukuruni kwa lipi – tazama ombi lake.

* Kwa nini Mfarisayo hakuweza kutaja chochote ambacho Mungu alimtendea?

* Je Mfarisayo alikuwa na mafundisha gani ya dini juu ya kuhesabiwa haki? (Tazama ujumbe ulioko mwanzoni.)

3. Ni wakati gani kama umewahi kuomba kama yule Mfarisayo katika mfano huu? ( Jibu moyoni mwako.)

* Kitenzi katika lugha ya Kiyuyani katika ombi la Mtosha ushuru una maan ifwatayayo: "Mungu, unihurumie kwa sababu ya kafara ambazo zinatolewa katika hekalu hii." Je mafundisho ya dini ya huyu mtosha ushuru yalikuwa yapi?

4. Ni kwa njia gani tunaweza kufanana na Mfarisayo katika mfano huu?

* Dhambi za Mfarisayo zilikuwa nini dhidi ya Mungu na jirani?

* Kwa nini Mfarisayo hakutambua hata dhambi moja yake?

5. Imani ya Mfarisayo ilikuwa imara kuliko ile ya mtosha ushuru. Kwa nini imani yao uongo huwa ina nguvu kuliko imani ya kweli?

6. Ni nani ambaye alijua kuwa miongoni mwa hawa wawili alikuwa mwenye haki walipoondoka Hekaluni? (Singatia somo!)

* Kwa nini Yesu hakumaliza mfano wake kwa kusema: "Na baada hayo, mtosha ushuru aliweza kufidia wale ambao aliwanyanganya pesa, na kubadilika kuwa mtu mwema."?

7. Mfarisayo bila shaka aliweza kuharibu maisha ya watu wengi. Ni nini kilifanyika kwa hukumu angalipata kutoka kwa Mungu kwa sababu ya dhambi zake?

8. Je mwenye kuhesabiwa haki ana changia nini katika kuhesabiwa haki?

* Je Mungu ana nafasi ipi katika kuhesabiwa haki?

* Je kafara ina nafasi gani katika kuhesabiwa haki?

HABARI NJEMA: Kafara ailiyotolewa Hekaluni ni picha ya kifo cha Yesu. Kwa kweli Mtosha ushuru aliomba msamaha kwa ajili ya kafara ya Yesu. Dhambi zake zilihesabiwa kwa Yesu wakati huohuo alipewa haki ya Yesu.

# 32. MTOSHA USHURU JUU YA MTI Luka 19:1-10

KUMBUKA: Siku za Yesu, watosha ushuru walifahamika kwa kutokuwa waaminifu. Walitosha ushuru zaidi kutoka kwa watu na kujiwekea sehemu kubwa kuliko walitakiwa. Kwa kawaida tunafikiri kuwa Yesu alikuwa upande wa walionekewa na masikini, na hapa tunaona yuko upande wa kumgandamizaji. Katika utamaduni wa Kiyahudi, kuingia katia nyumba ya mtu kwa chakula ilikuwa ni ishara ya urafiki.

1. Je maisha ya kila siku ya Zakayo yalikuaje, mku wa watosha ushuru Yeriko? Ni yalpi yalikuwa mazuri na mabaya?

2. Je Zakayo angali halalisha mwenendo wa biashara yake na mtindo wa maisha yake?

* Unafikiri ni kwa nini Zakayo alitaka pesa nyingi?

3. Unafikiri ni kwa nini Zakayo alitaka kumwona Yesu-toa ababu nyingi uwezavyo?

* Je unafikiri mkuu wa watosha ushuru angependa kuonekana akiwa juu ya mti? Toa sababu.

4. Kumbuka wakati mtu Fulani alichukua pesa zako kinyume na sharia. Kam ungalikuwa mmoja wapo wa wadhiriwa wa Zakayo, je ungechukuliaje tabia za Yesu katika mstari wa 5?

5. Je nini ambacho ni cha kushangaza juu ya Yesu kukutana na Zakayo mora ya kwanza-Kumbuka hii ilikuwa nia mara ya kwanza nay a Miwsho kuingia Yeriko?

6. Je unafikiri ni lini Zakayo alianza kumwamini Yesu (5-8)? Jadili uwezekano mbalimbali.

7. Je unafikiri Zakayo angalifanya nini kama Yesu angalisema, "Shuka chini mara moja na wape masikini nusu ya mali yako. Ndipo nije nyumbani kwako"?

* Ungefanya nini kama Yesu angalikwambia: "Kwanza tubu dhambi zako ndipo niwe rafiki yako"?

8. Ebu fikiri itakuwaje kama ungetoa nusu ya mali kwa siku mmoja. Ni nini kingelikufanya ufanye hivyo?

* Je Zakayo alipata nini badala ya hela aliyopoteza?

9. Kuna tufauti gani kati ya Zakayo na raia wa Yeriko? (Tazama mstari wa.7.)

* Kwa nini alitaka kumtembelea mtu mbaya katika mjiti?

10. Yesu anasema nawe leo: "Nitakuwa mgeni wako leo." Anataka kwenda nawe na kukaa katika nyumba yako. Utamjibu nini?

11. Ninani alimtafuta nani katika somo: Je Zakayo alikuwa anamtafuya Yesus au Yesu ndiye alikuwa namtafuta Zakayo? (3,9,10)?

HABARI NJEMA: Akiwa njiani kwenda Yerusalemu kwenda kusulupiwa, Yesu alipitia Yeriko. Pengine ni kwa ajili ya Zakayo. Yesus aliposamehe dhambi za Zakayo, alijua kuwa angalipata

adhabu yaye. Msamaha wa dhambi ni bure kwa ajili ya Zakayo na ni bure kwa ajili yetu- lakini limgharimu Yesu maisha yake.

# 33. MFANO WA MWISHO Luka 20:9-19

KUMBUKA: Misabibu ilinaanisha kwanza Wayahudi, kwa viongozi wao hasa, lakini sasa inamaanisha Kanisa la Kikristo katika nyakati za mwisho.

1. Je wapangaji wa ardhi walifikiri mweye shamba ni mtu wa aina gani?

* Je kosa la wapangaji lilikuwa nini juu ya mwenye shamba?

* Ni uhusiano aina gaki kati aya Munguna mwanadamu ambao Yesu anataka kuongeysha kwa mfano huu?

2. Kwa nini mwenye shamba hakuingialia mtumishi wa kwanza aliporudi mikono mitupu (10)?

* Je unafikiri ni kwa nini matendo ya wapanganji yaliendelea kuwa mabaya kila wakati (10-12)?

* Kwa nini Mungu hakuweza kuzuia watumishi wake kutendewa vibaya and kutezwa?

3. Je Mungu anatarajia matunda aina gani kutoka kwetu ?

* Ni matunda aina gani Mungu anatarajia kutoka Kanisa letu?

* Ni kwa sababu gani mara nyingi ni vigumu kumpa Mungu matunda ya kazi yetu?

4. Mwnye shamba alikuwa na kusudi gani alipo mtuma mwanae mpendwa shamabani?

* Ni kwa sababu gani unaweza kumtuma mwanao kwa mahali sawa sawa na hapo kwa hatari ya maisha yake.?

* Je ni kwa nini dunia ni muhimu kwa Mungu hadi Mungu kumtoa mwanae wa pekee hapa?

5. Ni nini kilichowafnya wapangaji kuwa na ujasiri hadi kumtuma mtoto wa Bwana wao?

* Ni nini kiliwafanya watu kuwa na ujasiri hadi kumuua mwana wa Mungu?

* Ni kwa njia gani tuko na hati kwa kifo cha Yesu?

6. Ni nini kitafanyika kwa wale wote ambao wana hatia katika kifo cha Yesu (16)?

* Je unaweza kuhuzisha matari wa 16 kwa Kanisa la Kikristo nyakati za mwisho?

7. Baada ya kumaliza mfano wa wapangaji Yeus alitumia picha inayofahamika kutabili juu ya kifo chake: jiwe la pembeni. Je mistari ya 17-18 inamaanisha nini?

* Ni nini kinachofanya Kanisa au mtu binafsi kutpa jiwe la pembeni la Imani yao?

8. Ni nini ambacho Yesu alitaka kusema kupitia mfano wake wa mwisho kwa viongozi wa Wayahudi?

* Je Yesu anataka kusema nini kwa viongozi wa Kanisa kupitia kwa mfano huu?

* Yesu anataka kusema nini kwawako kupita kwa mfano huu?

## 34. SADAKA YA MJANE Luka 21:1-4

KUMBUKA: Kuna ahadi nyingi kwa ajili ya wajane na yatima katika agano la Kale, kwa mfano Zaburi 10:14,17, 18 na 68:5. Pengine mjane katika somo letu alikuwa amesikia juu ya ahdi hizi. Sadaka zilitumika kwa ujenzi wa Hekalu, ambalo lilimalizika mnamo mwaka wa AD 63 na kuharibiwa AD 70 – miaka arobaini baada ya matukio haya.

1. Kwa nini watu hutoa sadaka katika dini zote?

* Marko katika masimulizi yake ya hadithi hii antwambia kwamba makusanyo yalikwekwa katik ahali ambayo inaonekana (Marko 12:41). Je mtoaji anaweza kuwa na uzawishi wa aiga gani kama watu wengine wangalifahamu mwishowe alitoa kiasi gani?

* Je mjane huru angalikuwa na mawazo gani kama angalifahamu kuwa Yeus alikuwa anamtazama kwa makini?

2. Jamni ya Kiyahudi hakuwa na mfuno wa utunzanjia wa kijamii na wala halikuwaruhusu wanawake kufanya kazi nje ya nyumbani. Fikiri ulikuwa umepoteza mme na unajaribu kulea watoto katika hali ile. Nini kingalikuwa kigumu kufanya?

* Kama ungalikuwa katika hali ilisemwa hapo juu, ungemtolea nani au kwa ajili ya kitu gani ungalitoa hela yako ya mwisho?

3. Ni nini kinachomfanya mtu kumtolea Mungu “vyote alivyo navyo ambavyo alitegemea” (4b)? Fikiria uwezekano mbali mbali.

4. Kama ungalimlazimisha mjane kuota hela yake ya miwsho, ungalifikiria nini juu ya Mungu wa aina hiyo?

* Je Imani ya hawa watu wawili ilitofautianje: Yule ambaye anamtolea Mungu huku aikiwa na shukrani kwa alivyo navyo na mwingine ambaye anamtolea ili kuweza kupata kitu kutoka kwake.?

5. Je Imani ya huyu mjane ilikuaje?

* Je huyu mjane alizawishikaje kuwa Mungu angetunza watoto wake?

* Je ni vigumu kwako kuamini kwamba Mungu atakutunza wewe na watoto wako kifedha pia?

6. Mjane huyu alikuwa amepata nini kutoka kwa Mungu?

* Je umepata nini kutoka kwa Mungu (linganisha na mjane huyu)?

7. Je unafikiri watoto wa mjane huyu walienda nyumbani bila chakula usiku ule? Toa sababu.

* NI nini unafikiri kina madhara kwa watoto wako/ wajukuu: Kwa wanaweza kutezeka kwa kukosa au au kupata kila ambacho wange kihitaji?

8. Je Mungu angependa umpe nini au jirani yako ambaye anatezekana leo? Unaweza kujibu katika moyo wako kama ungependa.

9. Je majane huyu aliwaachia nini watoto wake kama urithi?

* LInganisha urithi ambao matajiri katika somo hili walichia watoto wao na ule yule mjane aliacha.

* Je ungependa kuwaachia watoto wako nini utakapokufa?

HABARI NJEMA: Dhambi zetu zinalinganishwa na kiasi kikubwa cha pesa katika Biblia- talanta elifu kumi. Kila mmoja wetu ambaye hawezi kulipa atatupwa gerezani (k.m.. motoni). Yesu alipotaka kutununua kutoka deni kubwa alitoa “kila alichokuwa nacho tegemea” – na damu yake ya thamani.

## 35. PETRO ALIMKANA BWANA WAKE Luka 22:31-33 na 54-62

KUMBUKA: Kiongozi asome Mathayo 10:32-33 ili kila mmoja aweze kuelewa kuwa ni dhambi mbaya kiasi gani kukataa kwamba humjui Yesu mbele ya watu.

1. Kam mtu anayekupenda atatabili kwamba utajitenga naye siku Fulani, je utafanya nini?

* Kwa nini Petero hakuweza kuamini utabiri wa Yesu katika mstari wa 34?

2. Kwa nini Petro si kama wanfunzi wengine alimfuata Yeu hadi kule barza la kuhani mkuu?

3. Je Petero aliogopa nini alipomkana Yesu mara tatu?

* Ungalifanya nini kama ungalikuwa katika mahali pa Petero?

* Ni katika hali gani unafikiri ulijaribu kukana Imani yako ya Kikristo?

4. Katika msatari wa.61 maneno ya Yeus ya kumhaga Petro yanasemwa. Je unafikiri Yesu alitaka kusema nini kwa wanafunzi wake walioanguka kwa mtazamo wa mwisho?

* Ni nini kilichomfanya mtu mzaima kuslia sana (62)?

5. What did Peter think at this point about the conversation he had had with Jesus earlier on the day (31-34)?

* Je unafikiri ilimaanisha nini kwa Petro kufhamu kwamba Yeus alikuwa anamwombea?

6. Mapema, Petero alikataa kabisa kabisa walo la Yesu kuawa. Je alisoma nini kutoka na tukio hili kwa nini Yesu alihitaji kufa?

7. Jambo hili lilimfanyaje Petro kuna na uwezo wa kuwafariji ndugu zake?

* Je kunaguka kwetu katika dhambi kunawezaje kutufanya tuimalishe ndugu zna dada zetu?

8. Yesu anakuangali wkati huu jinsi alivyomwangalia Petro baada ya anguko lake. Je macho yake yanasema nini kwako?

HABARI NJEMA: Petro alimkana Bwana na mkubwa wake, lakini alisamehewa. Badala yake, Yesu aliweza kukutana na kukanwa na baba yake akiwa anachukua adhabu ya hofu yatu mslabani.

# 36. MILANGO YA PARADISO UMEFUNGULIWA  Luka 23:32-43

KUMBUKA: Wakati wa Yeus watu walisulubishwa kwa makossa makubwa tu. Tunaweza kusema wale wezi walisulubiwa kwa sababu ya pesa au walifanya makossa makubwa sana.

1. Ni nini ambacho kiliwafanya hawa wanaume wawili waanze kuiba na kupigana n.k? Fikiria sababu mbalimbali.

* Hawa wanaume wawili walikuwa na mama zao nap engine wake zao pia. Ebu fikiria maisha ya kila siku ya hao wanawake wawili.

* Kwa nini wezi hao hakuacha wizi kabla ya kufikia hapo walipo?

* Why don't we always stop the behaviour we know is harmful to ourselves and to others?

2. Hawa wawili waliona kusulubiwa kwa Yeu kwa karibu sana kuliko mtu yeyote. Ni nini katika maneno na matendo ya Yesu ilifanya usawishi mkubwa kwa mmoja wao (34-38)?

* Hawa wawili waliishi katika dunia ya chuki na kizazi. Je walikifiria nini juu ya maombi ya Yesus katika mst.34?

3. Ni nini kilichomfanya mmojawapo wa wanyanganyi kutambua dhambi zake?

* Nini ambacho kinatufanya kutambua dhambi zetu badala ya kuzitetea?

4. Ni nini kilicho mfanya mmoja wa wezi kutambua kwamba Yesu alikuwa mfalme (37,38,42)?

* Yesu alikuwa mfalme gani mda ule, ukilinganisha na wafalme wengine?

5. Kwa nini yule mwizi mwingine hakuamini kuwa Yesu alikuwa Kristo au mfalme?

* Kwa nini kutambua dhmabi kunazidi Imani ya kweli?

6. Katika mstari wa.42 tunapata ombi fupi: "Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako." Kwa nini huyu mwizi hakumwomba Mungu kumruhusu kuingia katika ufalme ule?

* Kwa nini ni faraja kufahamu kuwa kuna mpendwa wetu anatukumbuka tunapotezeka?

* Kwa nini huyu mwizi alitaka Yesu amkubuke, muuaji wakati angetezeka jehanamu?

* Ni katika hali gani unafikiri wewe mwenyewe ukiomba ombi hilo?

7. Mwizi huyu aliokolewa lini?

* Ni nini kilitendeka na dhambi za mtu huyu?

8. Msiaha ya Mkristo yalikuwa mafupi kulingana na mwizi huyu, yaa masaa sita tu. Je unafikiri alikuwa na furaha au hakuwa katika masaa ya mwisho?

* Je unafikiri huyu mtu alimchukia mtu fulani katika mda wake wa kufa?

* Kibinadamu huyu mwizi aliharibu maisha yake. Na bado maisha yake yaliyakikisha kuwa muhimu?

HABARI NJEMA: Milango ya Paradiso ilifungwa tangu siku za Adamu na Hawa. Sasa malango ulifunguliwa kwa muuaji. Mda huo huo mlango ulifungwa kwa Yesu, ambaye alihitajika kuingia katika milango ya Jehanamu.

# 37. MATEMBEZI YA KWENDA EMAU     Luka 24:13-35

KUMBUKA: Emau ilikuwa ni mji ambalo ulikuwa 11 kilometa kutoka Yerusalemu. Ilichukua angalau masaa mawili kutembea umbali huu. Mariamu mke wa Clopa, alitajwa kama mmoja wa wanawake ambao walisimama karibu na msalaba Yesu alipokufa (Yohana 19:25). Inawezekana ni mke wa Cleopa ambaye anatajwa katika somo hili.

1. Kama umewahi kuteza mtu ambaye unampenda, unajua ni mawazo ya aina gani, hisia na majuto ambayo unakaa nayo baada ya mazishi. Simulia.

*Yesu alikufa siku mbili zilizopita katika kifo cha uchungu. Je unafikiri ni nini ambacho kilikuwa kigumu kwa Kleopa na marafiki zake siku zile?

2. Kwa nini Yesu aliwaruhus kwanza hawa wanaume wawili waombolezaji kuongea juu ya uchungu wao (15-17)?

* Ni nini kingalifanyika kama Yesu angalianza kuwambia juu ya maelezo ya Bibilia moja kwa moja?

* Yesu anajua masikitiko yetu tayari –Kwa nini anapenda kuyasikia kutoka vinywa veytu?

3. Je imani ya hao wanaume wawili ilibadilikaje baada ya kifo cha Yesu (19-21)?

* Kwa nini hawa watu wawili hakuamini yale mbayo wanawake na wengine waliwambia juu ya kufufuka (22-24)?

4. Je kuna tofauti gani kati ya tafsiri Yesu anayoitoa juu ya kifo chake na ile Kleopa na rafiki yake walitoa (19-21 na 25-27)?

5. Kwa nini Kleopa hakuelewa kutoka Moses na Manabii (k.m. Biblia) kwamba ilikuwa lazima Kirsto kutezeka na kufa?

6. Kwa nini Yesu alijifanya kana kwamba anawapita kwenda mbali (28)?

7. Kwa nini hawa wanaume wawili hawakutambua Yesu alikuwa nani hadi alipomega mkate?

8. Ni nini kilichowafanya hao wanaume wawili kutembea umbali wa kilometa 11 kurudi Yerusalemu katika giza?

9. Katika siku zetu watu wengi ambao wanajiita Wakristo hawamini kufufuka kwa mwili kwa Yesu. Ni Mungu wa aina gani hawa watu wanaamini?

* Ni kwa nini mtu hawezi kuwa Mkristo kama aamini kufufuka kwa mwili kwa Yesu Kristo?

HABARI NJEMA: Yesu alimega mkate katika nyumba ya Kleopa kwa mikono yake iliyokuwa na alama. Hawa wanaume waili wangalimtambua Yeus kwa alama ya vidonda. Tunaweza kukutana na Kristo mfufuka kwa njia sawa na ile kila mara tunaposhiriki katika meza ya Bwana.

# 38. KWA MATAIFA YOTE   Luka 24:44-53

1. Kulinagana na Yesu, ni ujumbe gani wanfunzi wake wanahitaji kuhubiri na watahubiri wapi?

* Kwa nini Yesu aliwapa huduma hii kwa wanaume kumi na moja ambao hawakuwa na elimu?

2. Ni mabo gani ambayo yalifungua mawazo ya wanafunzi kuelewa Agano la Kale?

* Ni nini kitafanyaki kwetu ili tuweze kuelewa Agano la Kale?

3. Yesu anawaita wanafunzi wake mashahidi (48). Je wanshuhudia nini?

* Tunahitaji kushuhudia nini na kwa nani?

4. Neno "Shahidi" inaweza kutafsiriwa kuwa "mfia dini". Ni nini kiliwafanya wanfunzi kuwa tayari kufa kwa ajili ya injili?

5. Yesu anawahidi wanfunzi wake nguvu kutoka juu. Kwa nini nguvu hii ni sharti kwa wanafunzi wa Yesu?

* Je unafikiri unapeta nguvu kutoka juu na kama ni ndio kwa njia ipi?

6. Paulo mmisionari mkuu, anaelezea nguvu hii kutoka juu akma igwtavyo: (Kiongozi asome Warumi 1:16 na 2.Wakorintho 12:9-10.) Jadili: nguvu ya Mungu ainatofautianaje na maana ya kawadia ya neon “nguvu”?

7. Kulingana na somo hili, je kuna masharti gani ya kuwa mmisionari?

8. Kwa nini Yesu hakuishi katika hali yake ya kimwili hapa duniani?

* Je kupaa kulitokeaje?

* Ni nini kiliwafanya wanfuzi kuwa na kuwa na furaha hata ingawa Bwana wao alitolewa kwao?

9. Jadili: Je ilikuwa ni raisi kwa wanfunzi kuweza kuwasiliana na Yesu baadaya ya kupaa, kama vile ilikuwakuwa akiwa bado duniani?

* Je unatambua mara kwa mara kuwa Yesu yu karibu nawe kam rafiki asiyeonekana?

HABARI NJEMA: Juu yay ale Yesu anafanya mbinguni sasa soma. Waebrania 7:25.